

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 19 Juni, 2015

(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu, swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Limbu.

Na. 224

Mradi wa Kupandishwa Hadhi Barabara kuwa za Mkoa

MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU (K.n.y. MHE. DEO K. SANGA) aliuliza:-

Tuliomba barabara ya kutoka Mtwango kupitia Kichiwa hadi Ikuna Nyombo, pia barabara ya kutoka Makambako-Mlowa-Manga-Usetuke-Kifumbe-Ibatu-Itandililo kuunganishwa na barabara ya Mgololo:-

- (a) Je, ni lini barabara hizo zitapandishwa hadhi kuwa za Mkoa?
- (b) Je, ni lini zitaanza kutengenezwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Njombe Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Njombe kilichofanyika tarehe 04 Juni, 2012, kilipendekeza barabara za kupandishwa hadhi kama ifuatavyo:-

- (i) Mtwanga-Kichiwa-Ikuna hadi Nyombo yenye kilomita 28.6;
- (ii) Makambako – Mlowa – Manga – Kifumba - Kichiwa hadi Kitandulilo yenye kilomita 35;
- (iii) Mfiliga – Ikangasi - Itambo hadi Idete yenye kilomita 65; na
- (iv) Makambako - Usetule hadi Kitandililo yenye kilomita 34.

Mheshimiwa Spika, hapo tarehe 30 Julai, 2013, Mkuu wa Mkoa wa Njombe alimwandikia Waziri wa Ujenzi barua yenye Kumb. Na. CA.204/311/01A/21 ya kuomba kupandishwa hadhi kwa barabara hizo. Aidha, wataalam kutoka Wizara ya Ujenzi walifika Njombe na kufanya ukaguzi wa barabara hizo kuanzia tarehe 13 hadi 23 Novemba, 2014 kuona kama zinakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi. Hivyo, Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Ujenzi kwa kushirikiana na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe ili kupata majibu ya maombi hayo ya kupandishwa hadhi barabara hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara hizi zinaendelea kufanyiwa matengenezo ya kawaida na Halmashauri za Mji wa Makambako pamoja na Halmahauri ya Wilaya ya Njombe hadi hapo zitakapokuwa zimekabidhiwa kwa TANROADS na kuingizwa katika bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Katika mwaka wa Fedha 2014/2015, jumla ya shilingi milioni 297 zilitengwa kutumika kwa ajili ya barabara hizo.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Limbu maswali ya nyongeza.

MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara zilizotajwa tatu kutoka Mtwango kwenda Ikuna - Nyombo na kutoka Makambako – Mlowa - Manga hadi Ibatu - Kitandililo zilipitishwa kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Njombe tarehe 04 Juni, 2013 na mwezi mmoja baadaye Mkuu wa Mkoa wa Njombe alimwandikia barua Waziri wa Ujenzi ili kuomba kupandishwa hadhi kwa barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini ilichukua mwaka mzima hadi wataalam kutoka Wizara ya Ujenzi kwenda Njombe kufanya ukaguzi...

SPIKA: Naomba ufike kwenye swali maana sasa ni hotuba.

MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Spika, Serikali inasema bado Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Ujenzi, kwa mwaka mzima inaendelea kufanya mawasiliano. Mheshimiwa Waziri aseme ni lini utaratibu huu wa kuwasiliana utakafikia mwisho na hatimaye wananchi hawa wapandishiwe hadhi barabara hizi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kanuni kwamba Makao Makuu ya Mkoa, moja, lazima yaunganishwe na barabara ya lami na Makao Makuu ya Mkoa mwingine. Je, ni lini barabara ya kuunganisha Mkoa wa Mwanza na Simiyu pale Bariadi utajengwa kwa lami? Ahsante.

SPIKA: Ahsante kwa kupenyeza, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. (Kicheko)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, sheria inayozungumzwa hapa ni Sheria Na.13 ya mwaka 2007, ndiyo inayoweka mamlaka na madaraka yote ya kupandisha hadhi hizi barabara ziwe za lami na kwa kiwango hicho cha TANROADS mikononi mwa Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, sisi hapa siyo kwamba hatukufanya kazi yetu, tumefanya kabisa, nimeongea na mtu wa TANROADS kutoka katika Mkoa wenu kule, nikamuuliza kwamba mmefikia wapi, tumejaribu kumtafuta na Katibu Mkuu mwaka mzima umepita. Walichoniambia si kwamba tunashughulikia barabara za Njombe na Makambako tu bali zinashughulikiwa za nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, alichofanya Waziri huyu ni kwamba ameunda timu ambayo inakwenda nchi nzima ili iweze ku-compile na kumpeleka mapendekezo ili aweze kufika mahali afanye maamuzi kuhusu jambo hilo. *Mandate* na *power* ya kwamba yeye anafanya hivyo kwa muda gani haipo mikononi mwetu bali ipo mikononi mwa Waziri mwenye dhamana ambaye ni Waziri wa Ujenzi. Kwa vile nazungumza kwa niaba ya Serikali, nataka niseme nitalifikisha jambo hili kwake ili tuweze kujua vizuri kwamba maombi haya lini yatakuwa yamefanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, ametaja hii barabara nyingine ya Mwanza inayokwenda mpaka Simiyu, barabara hii haipo chini ya halmashauri, nimeshaipitia barabara hiyo. Hata hivyo, hili nalo nitalifikisha ili tuone inajengwa kwa kiwango cha lami kama Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu anavyopendekeza.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Malocha swali la nyongeza, nilifikiri nimemwona, hayupo? Haya tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, kwa niaba yake Mheshimiwa Abdulsalaam Selemani Amer.

Na. 225

Barabara ya Vigwaza Kupewa Hadhi ya Kuwa ya Mkoa

MHE. ABDULASALAAM S. AMER (K.n.y. MHE. HAMOUD A. JUMAA) aliuliza:-

Ombi la barabara ya Vigwaza kupewa hadhi ya kuwa barabara ya Mkoa ni la muda mrefu sana lakini hadi sasa ombi hilo bado halijapatiwa ufumbuzi:-

Je, ni lini barabara hii itapandishwa hadhi na kuwa barabara ya Mkoa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, barabara ya Vigwaza - Dutumi-Kimaramisale, inaunganisha Halmashauri za Wilaya za Bagamoyo (Vigwaza-daraja la Msua km.9), Kibaha (daraja la Msua-Dutumi km.22.6) na Kisarawe (Dutumi-Kimaramisale km.17)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha katika kikao chake cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) kilichofanyika tarehe 5 Desemba, 2013 kilipitisha pandekezo la kupandishwa hadhi barabara hiyo kuwa ya Mkoa na iliwasilisha pandekezo hilo kwa Katibu Tawala Mkoa kwa ajili ya kulipeleka kujadiliwa katika kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Pwani kilichofanyika tarehe 1 Desemba, 2014, Wajumbe walijadili suala la barabara hii ili iweze kupandishwa hadhi. Kwa pamoja walikubaliana kuwa haitaombewa kibali kwa sasa kwa sababu barabara nyingi zimekuwa zikipandishwa hadhi lakini hazipati fedha. Hii imesababisha barabara hizo kutotengewa fedha na Halmashauri husika. Hivyo, kikao kiliamua barabara hii iendelee kuhudumiwa na Halmashauri zote tatu na kuziagiza kuitengea fedha za matengenezo katika bajeti ya 2015/2016.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, barabara hizo zimetengewa fedha katika mwaka 2015/2016 kama ifuatavyo:-

JINA LA HALMASHAURI	ENEO LA KUTENGENEZA	FEDHA ZILIZOTENGWA
Bagamoyo DC	Vigwaza hadi Daraja la Msua	24,000,000.00
Kibaha DC	Daraja la Msua hadi Dutumi	172,000,000.00
Kisarawe DC	Dutumi hadi Kimaramisale	34,140,000.00
JUMLA KUU		230,140,000.00

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Abdulsalaam.

MHE. ABDULSALAAM S. AMER: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, tatizo la barabara nchini liko kila sehemu, kwa mfano kwenye Wilaya yangu ya Kilosa, Jimbo la Mikumi kuna barabara ya kutokea Ruaha Mbuyuni hadi Malolo kuelekea Wilaya ya Mpwapwa, ni kiunganisha kati ya Wilaya ya Kilosa na Mpwapwa. Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi barabara hizi kwa nchi nzima ambazo tunahitaji ziwe chini ya *TANROADS*?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, barabara hii anayoisema anapendekeza iwe *TANROADS*, nitakachofanya hapa, kwa sababu mimi sikujua kwamba swali hili litaulizwa, nitakwenda kuangalia orodha yote ya barabara zilizoombewa na kuona *status* yake ili kama itaonekana kwamba imekwenda niweze kufuatilia katika Wizara ya Ujenzi ambayo ndiyo yenye dhamana ya kusema hii tumekubali na hii tumekataa.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mangungu swali lingine la nyongeza, hizo balaghashia zinanifanya nisiwajue. (*Kicheko*)

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, mfungo huu. Napenda nimuulize swali la nyongeza Mheshimiwa Waziri kwamba barabara ya kutoka Njia Nne hadi Kipatimu ambayo yeye mwenyewe aliipita wakati alipofanya ziara katika Jimbo hili na barabara ya Nangurukuru - Njinjo - Miguruwe alipita vilevile kwenye ziara. Ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha ili ijengwe kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, barabara hizi zote anazosisema Mheshimiwa Mangungu ni kweli mimi nimezipita nimeziona. Kitu ambacho naweza nikamwomba Mheshimiwa Mangungu pamoja na Wabunge wengine wote, kesho kutwa tunakuja kupitisha bajeti hapa, nawaomba wote tuseme ndiyo ili fedha hizi zikipita pamoja na hizi barabara ambazo Mheshimiwa Mangungu anazosisema ziweze kupatiwa fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo ambayo naweza nikayasema kwa sasa.

SPIKA: Ahsante. Tuendeleo na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza atauliza swali, kwa niaba yake Mheshimiwa Moses Machali.

Na. 226

Nyumba Bora kwa Askari Polisi na Magereza Manispaa ya Bukoba

MHE. MOSES J. MACHALI (K.n.y. MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA) aliuliza:-

Nyumba za Askari wa Polisi na Magereza zilizoko kwenye eneo la Nshambya na Miembeni katika Manispaa ya Bukoba ni za miaka mingi na zimechakaa sana:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Askari hao makazi bora?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyowahi kujibu maswali kadhaa ndani ya Bunge lako Tukufu kuhusu uhaba na uchakavu wa nyumba za Askari hapa nchini, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa nyumba za Askari Magereza

na Polisi zilizopo eneo la Nshambya na Miembeni katika Manispaa ya Bukoba ni za miaka mingi na zimechakaa sana.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya nyumba kwa Askari ni makubwa ambapo uwezo wa Serikali kufanikisha ujenzi wa nyumba hizo kwa wakati mmoja ni mdogo. Ili kupambana na tatizo hili Jeshi la Magereza limepanga kulifanyia ukarabati jengo la ghorofa nne linalokaliwa na familia 72 lililopo katika Kata ya Miembeni katika Manispaa ya Bukoba. Ukarabati huo utahusisha kupaka rangi, kurekebisha mfumo wa maji taka, maji safi na umeme katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha endapo Serikali italipatia Jeshi fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchakavu mkubwa wa nyumba za Polisi eneo la Nshambya, Serikali haina mpango wa kukarabati nyumba hizo kwa sasa isipokuwa nguvu kubwa imeelekezwa kwenye ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la ghorofa tatu lenye uwezo wa kuchukua familia 36 eneo la Byekera. Pia, Serikali iko mbioni kujenga maghorofa mawili yenye uwezo wa kuchukua familia 24 eneo la Nshambya ilipo Kambi ya FFU Bukoba Mjini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na juhudi za kutatua tatizo hili nje ya utaratibu wa kawaida wa kibajeti kwa kushirikiana na wadau mbalimbali chini ya mpango shirikishi wa PPP.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Moses Machali maswali ya nyongeza.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Serikali inakiri kwamba ina uwezo mdogo wa kujenga nyumba za kutosha kwa ajili ya Askari Polisi na Magereza lakini inafahamika bayana kwamba Magereza zetu zimesheheni rasilimali watu ambayo pengine ingeweza kutumika kikamilifu kutatua tatizo hili kwa kiwango fulani. Kwa nini Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani isiwe na mpango mkakati wa kuhakikisha inawatumia kikamilifu wafungwa waliopo magereza ili wafyatue tofali na hatimaye kujenga nyumba za Askari, Polisi na Magereza ili kupunguza mzigo kwa Serikali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Askari hawa walistahili kupewa makazi wakae kambini ili ku-*maintain* suala la nidhamu miongoni mwa Askari. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipia Askari wote ambao hawana makazi nyumba ambazo wanaishi huko mitaani?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, wazo la kutumia wafungwa siyo jipya na ni kweli kwamba wafungwa wanatumika katika ujenzi wa nyumba hasa za Magereza wenyewe. Uwezekano wa kujenga nyumba nyingine upo lakini ujenzi hautamalizika kwa kutumia rasilimali watu lazima vifaa vipatikane ndiyo wao wafanye kazi. Tatizo kubwa ni kwamba hili jambo ni la muda mrefu halikushughulikiwa ipasavyo na limekuwa limbikizo la tatizo. Kwa hiyo, tukipata vifaa, nguvukazi ya Magereza au wafungwa itasaidia.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kuhusu makazi ya Askari, Askari wote ambao wameorodheshwa kwenye kazi wanalipiwa nyumba kupitia kwenye mishahara yao.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Ole-Medeye.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ina vituo kadhaa vya Polisi lakini kwanza, nikiri Serikali inafanya kazi nzuri ya kujenga nyumba za Polisi Mkoani Dar es Salaam na maeneo mengine lakini ukienda Mkoani Arusha zile alizotuachia mkoloni ndizo tulizonazo na hazijafanyiwa ukarabati zimechoka lakini Askari wetu bado wanaendelea kuishi humo.

Mheshimiwa Spika, tuna Kituo cha Oldonyosambu na Ngaramtoni, nyumba zilizopo pale zimechakaa sana kwa maana ya majengo ya ofisi pamoja na majengo ya kuishi. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba mpya katika kituo cha Polisi Ngaramtoni pamoja na Oldonyosambu ili kuwawezesha Polisi ambao nawapongeza sana kwa kazi wanayofanya...

SPIKA: Ni wakati wa kipindi cha maswali siyo hotuba.

MHE. GOODLUCK J. MEDEYE: Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za kuishi Askari pamoja na majengo ya ofisi katika Kituo cha Polisi Oldonyosambu na Ngaramtoni?

SPIKA: Inatosha kabisa, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Serikali mpango wake ni kujenga nyumba za Askari na vituo vipya nchi nzima. Ngaramtoni ni sehemu ya nchi hii na mipango inayoendelea kupangwa na jitihada ambazo zipo hasa za kutumia *private sector* pamoja na bajeti ya Serikali zitafanya siku moja tujenge Oldonyosambu na Ngaramtoni.

SPIKA: Mheshimiwa Mwidau swali la nyongeza.

MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali hili la Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza linafanana sana na hali iliyopo katika Wilaya ya Pangani. Nyumba zile za Polisi na Magereza, kwa kweli Mheshimiwa Waziri hali ni mbaya sana. Kama ulivyokiri kuwa unajua hali za nyumba za Polisi ni mbaya, Pangani tuna eneo tayari kwa ajili ya kujenga nyumba za Magereza. Mheshimiwa Waziri atuambie hapa, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea Polisi na Magereza katika maeneo ambayo tayari wameshajitolea na maeneo wanayo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, swali linarudia hilohilo tu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, mpango ndiyo uleule wa Ngaramtoni na Oldonyosambu. Ni kwamba sasa hivi kuna nyumba ambazo zinaendelea kukarabatiwa kwa uwezo ambao upo. Kuna mpango huu wa maghorofa ambao unaenea mpaka umefika Limbani na Chakechake Pemba. Mpango huu utafika Pangani ili mradi tustahimili kwa sababu hatuwezi kuji-*stretch* moja kwa moja kila mahali. Hivi sasa kuna mpango mwingine unakuja na Serikali ya China huenda kukapatikana nyumba kama 4,000 na zitaenea maeneo ya Pangani na kwingineko.

SPIKA: Naomba tuendelee na swali lingine, nyumba zote ni mbovu kwa hiyo mpango huo ufanyike. Naomba tuendelee na swali linafuata la Mheshimiwa Vicent Nyerere kwa niaba yake Mheshimiwa Christowaja Mtinda.

Na. 227

Jeshi la Polisi Kuajiri angalau Vijana 30,000 kwa Mwaka

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA (K.n.y. VICENT J. NYERERE) aliuliza:-

Uchumi wa nchi unakua kwa asilimia saba (7%) kwa mwaka lakini hakuna uwiano mzuri wa kimataifa kati ya polisi na raia na vijana wengi wapo tayari kujunga na Jeshi la Polisi:-

Je, ni lini Jeshi la Polisi litaajiri vijana 30,000 kwa mwaka?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vicent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba uwiano wa Askari Polisi na raia hapa nchini hauendani na viwango vya uwiano wa kimataifa ambao ni askari mmoja kwa raia 400. Ili kuboresha uwiano huu, Jeshi la Polisi limeendelea kuajiri Askari wapya kila mwaka kulingana na bajeti, ikama ya ajira na uwezo wa vyuo vya polisi kupokea na kutoa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Jeshi la Polisi lina jumla Askari 43,231 na ajira zinaendelea kufanywa kwa wastani wa Askari 3,000 kwa mwaka. Idadi hiyo inafanya uwiano wa sasa kuwa Askari mmoja kwa takribani raia 1,040. Aidha, jumla Askari wanafunzi 3,186 wako chuoni hivi sasa na wanatarajia kuhitimu mafunzo hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, pia Jeshi la Polisi liko kwenye mchakato wa kuajiri Askari 3,000 kabla ya mwezi Agosti mwaka huu hivyo tunatarajia kuwa na Askari takribani 49,500 ifikapo mwezi Desemba, mwaka huu. Idadi hiyo itafanya Askari mmoja kulinda wastani wa wananchi 950. Serikali itaendelea kuongeza idadi ya Askari ili kufikia viwango stahiki.

SPIKA: Mheshimiwa Christowaja swali la nyongeza.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Askari wetu wanalemewa na uwiano uliopo na alivyosema kwamba mpaka kufikia Desemba mwaka huu 2015 angalau Askari mmoja atalinda raia 950. Sasa swali langu la kwanza ni kwamba kwa uhalifu huu ambao unaendelea kuikumba nchi yetu ya Tanzania na kwa idadi hii ndogo ya Polisi ambao wanalinda raia wa nchi hii, je, Serikali haioni inatakiwa sasa iweke kipaumbele kikubwa katika kuongeza idadi ya Askari ili kuweza kupunguza uhalifu huu ambao sasa umekuwa ni fishio kwa nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa kuna vijana waliohitimu mafunzo ya JKT na wako mitaani na vijana hawa wamefundishwa mafunzo ya ulinzi na kutumia silaha, je, Serikali haioni sasa ni wakati muhimu wa kuweza kuwachukua hata hawa vijana waliofanya mafunzo ya JKT na kuwapeleka kwenye mafunzo ya Polisi kwa muda mchache ili waweze kupewa ajira na kulinda raia wetu?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kuhusu wimbi la uhalifu na kuongeza idadi ya Askari, kwa kiasi kidogo kuongeza Askari kunaweza kukapunguza wimbi la uhalifu lakini kwa kiasi kikubwa wimbi la uhalifu

haliwezi kupungua kwa nyongeza tu ya Askari. Haya mambo mengine wakati Askari wetu idadi yake ni ndogo ndiyo ya kuyashughulikia. Kuna mambo ya Polisi Jamii, kuna utayari wa wananchi kutoa taarifa, haya ndiyo mambo yatakayotulinda. Pia kila mwanafamilia kuhakikisha kwamba kwenye familia hakuna mhalifu, hayo ndiyo yatakayotusaidia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana waliopata mafunzo ya JKT, ni kweli kwamba wapo na hata hivi sasa kuna *rotation* ya tangazo la ajira ya Polisi. Kwa hiyo, nafikiri wanaweza wakaomba kama raia wengine wakapembuliwa na wale ambao wata-*qualify* wataajiriwa.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Askari mmoja analinda raia 1,040 na ametuambia kwamba ifikapo Desemba 2015 Askari mmoja atalinda raia 950 na *standard* ya kimataifa inasema Askari mmoja alinde raia 400. Nataka kujua sababu inayosababisha kuwepo na upungufu wa Askari Polisi? Ni kwa sababu Watanzania wengi hawataki kujiunga na fani hii ya Polisi kwa sababu haina tija au ni Serikali haina fedha za kuwapeleka Watanzania kusomea fani hii ya Polisi?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Watanzania wanalipenda Jeshi la Polisi na wengi wanaamini kwamba Polisi ina tija. Hii inathibitishwa nafasi chache zinazotangazwa kwa Watanzania wengi kuomba. Tatizo hasa ni miundombinu na *resources* za kuhakikisha kwamba tunaweza tukawafunza Askari wengi kwa wakati mmoja. Askari 3,000 ukienda pale Chuo cha Polisi Moshi utajua ni kundi kubwa na huduma zake pia.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba tunaajiri na kwa mwaka Serikali inatoa ikama ambayo lazima tuitimize. Tutaendelea kushauriana ili tuongeze idadi kwa mwaka lakini hatuwezi kama swali la msingi lilivyo tukaajiri Askari 30,000 kwa mara moja, uwezo huo kwa mwaka hautakuwepo.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tuendeleo na swali linalofuata, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya.

Na. 228

Kuchoma na Kuharibu Nyumba na Mali za Wawekezaji

MHE. MUHAMMED IBRAHIM SANYA aliuliza:-

Wawekezaji wengi wameonyesha dhamira ya kuwekeza katika sekta ya kilimo na viwanda hapa nchini; na wengi wa hao wawekezaji tayari wako nchini wanaendelea na shughuli zao lakini baadhi ya wananchi wamekuwa wakichoma moto nyumba zao na mali zao:-

Je, Serikali inawachukulia hatua gani wananchi wanaofanya uhalifu huo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na migogoro ya mara kwa mara hapa nchi ikihusisha wawekezaji na wananchi kwa kugombania maeneo hasa katika Mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro na mikoa yenye shughuli za uchimbaji wa dhahabu kwa mfano Geita. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge, mara nyingi migogoro hii hupelekea kuchoma moto au kuharibu mali za wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, migogoro hii imekuwa ikishughulikiwa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wananchi wa eneo husika faida ya kuwa na uwekezaji lakini pia kuwakutanisha pamoja kati ya mwekezaji na wananchi ili kutafuta muafaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati za Ulinzi na Usalama kuanzia ngazi za Wilaya hadi Mikoa zimekuwa zikifanya kazi hiyo na pale inaposhindikana basi mashauri hayo hupelekwa Mahakamani ili kutolewa uamuzi wa kisheria. Pamoja na jitihada hizo, wahalifu hufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Sanya maswali ya nyongeza.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania imejitangaza huko duniani kwamba ni mahali salama na pa amani kwa wawekezaji wa aina zote. Kwa kuwa kuna baadhi ya watu wameonyesha hamu na wapo nchini kuwekeza

hasa katika sekta ya kilimo. Je, Mheshimiwa Waziri anayo taarifa kwamba kuna mwekezaji mmoja wa kilimo katika Jimbo la Babati ambaye ameshavamiwa zaidi ya mara mbili na kuharibiwa mali zake na hata kuhatarisha usalama wake? Serikali imelifuatilia vipi suala hili ili mwekezaji huyu awe salama kwa sababu anachokifanya ni kuzalisha kwa ajili ya nchi na kwa ajili yake na hataondoka na ardhi hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali kabla ya kufanya taratibu za wawekezaji kuja nchini kwamba wametangaza biashara hiyo ifanyike au uwekezaji huo ufanyike, je, Wizara ya Mambo ya Ndani inahusishwaje na wawekezaji mbalimbali hasa katika maeneo ambayo huwa wanahatarisha usalama wao na mali zao na fedha zao ambazo ni nyingi na za kigeni katika nchi hii wanapokuja kuwekeza ili wawe salama na kuitangaza Tanzania kuwafanya wengine waje zaidi kuja kuwekeza katika nchi yetu?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Tanzania ni salama na tunaendelea kuwahimiza wawekezaji waje ili watusaidie kwa faida za uwekezaji ambazo zinatokea.

Mheshimiwa Spika, naelewa na nina taarifa ya mwekezaji ambaye amepata matatizo mara nyingi pale Babati na Serikali ipo katika kulitafutia ufumbuzi tatizo hili. Mara nyingi Serikali imefika pale kushuhudia lakini pia kutoa ushauri na kujaribu kupatanisha jambo hili. Mgogoro huu umekuwa mkubwa lakini Serikali bado inaendelea kuufanyia kazi na hatma yake nina hakika kwamba utakuwa salama na wananchi wataelewa faida ya mwekezaji au vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Wizara inashirikishwaji kabla ya uwekezaji, Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi zinahusika moja kwa moja katika masuala hayo ya ulinzi lakini pia katika uwezeshaji wa wawekezaji kuja nchini na kufanya kazi kwa mujibu wa sheria. Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji wanashirikishwa kupitia *One Stop Center* pale TIC Dar es Salaam au mikoani ambako ni sehemu kubwa katika sekta ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara inashiriki na kazi yake kubwa ni kuhakikisha kwamba usalama upo. Mara nyingi hawa wawekezaji hawatumii Askari Polisi katika kuhakikisha kwamba wana ulinzi wa kutosha lakini kuna ulinzi ambao ni *private* kutoka Suma-JKT na kampuni zingine ambazo kimsingi zinapata mafunzo kupitia Polisi wanashiriki katika kuhakikisha kwamba mali hizo na wawekezaji wenyewe wako salama.

SPIKA: Mheshimiwa Eng. Mnyaa.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri amesema njia moja ya kuondoa migogoro ya wawekezaji na wananchi ni kuwakutanisha wawekezaji na wananchi. Kwa kuwa katika hali kama hiyo ndiyo chanzo cha mgogoro na kwa kuwa maslahi ya wananchi wa Tanzania yanalindwa na Serikali yao na kwa kuwa wananchi taratibu nyingine za kisheria na za kiuwekezaji wao ni wageni wa taratibu hizo. Ni kwa nini basi Serikali isiwawekee masharti kabla yanayojulikana wawekezaji wote wanapokuja kuwekeza nchini uhusiano wao na wananchi nini cha kufanya, ili mwekezaji akajipima anaweza masharti hayo na kama anaweza kuwekeza au la?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Tanzania na nchi nyingi zinapotangaza nafasi za uwekezaji pia hutangaza taratibu za kufuatwa mpaka kuwekeza. Taratibu hizo pia zinajumuisha masharti yakiwemo ya kifedha, ya kijamii na kadhalika. Moja katika sharti kubwa ni kuhakikisha kwamba wanakuwa na *good neighborhood* na wananchi, hicho kitu kipo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na utaratibu huo bado kunatokea migogoro. Hii migogoro inawezekana inatokea kutokana na kutotimizwa kwa masharti upande wa mwekezaji na wakati mwingine upande wa wananchi. Kwa hiyo, ili kusawazisha hatuwezi kwenda moja kwa moja tukasema mkosaji ni huyu au huyu lakini ni kutafuta ukweli kwa kuwakutanisha na mara nyingine kutafuta *compromise* nje ya masharti kulegeza kidogo lakini wakati mwingine kusimamia sheria na kila mtu akapata haki iliyokuwepo.

SPIKA: Ahsante. Tuendeleo na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba atauliza swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Mtemi Chenge.

Na. 229

Maeneo ya Wachimbaji Wadogo

MHE. ANDREW J. CHENGE (K.n.y. MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA) aliuliza:-

Mheshimiwa Rais katika mkutano wa hadhara mwaka 2010 aliwaahidi wachimbaji wadogo wa Kijiji cha Nyarugusu kuwa watatengewa maeneo ya uchimbaji:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kujibu swali namba 229, kuna neno moja naomba niliseme.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza wananchi wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Jana nilikuwa Mufindi na Mufindi Kusini, nimewaona watu wa Mwenga na Mpanga, hawa watu ni wazuri sana. Wana mitambo midogo ya kuzalisha umeme ambayo kwa ujumla wake itaingiza kwenye gridi zaidi ya *megawatt* 200. Ahsante sana watu wa Mwenga. Jana pia nimezindua mradi wa kusambaza umeme vijiji 18 wenye thamani ya shilingi bilioni 10. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba, kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika katika kutenga na kugawa maeneo ya wachimbaji wadogo huanza kwa Wizara kubainisha maeneo yaliyo wazi na yanayofaa kwa wachimbaji wadogo yakiwemo yaliyofanyiwa utafiti wa awali na kurejeshwa na wawekezaji wakubwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuwa maeneo mengi katika Kanda ya Ziwa Victoria yapo ndani ya leseni kubwa za utafutaji madini, Wizara imefanya mazungumzo ili kufikia muafaka na baadhi ya wamiliki wa leseni hizo ambapo wenye leseni wakikubali kwa hiari yao wataachia baadhi ya maeneo ambayo hatimaye tutawagawia wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009 Serikali ilitenga kuyagawa maeneo mawili ya uchimbaji mdogo wa dhahabu katika Wilaya ya Geita; maeneo hayo ni Rwangasa hekta 710, Nyarugusu hekta 510. Maeneo

yote yalitengwa baada ya kampuni ya *IAMGOLD Tanzania Ltd* kukubali kuyaachia ili yagawiwe kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2010 – 2015, pamoja na mambo mengine, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Madini ya mwaka 2009 na Sheria ya Madini ya mwaka 2010 zinazoelekeza kuwaendeleza wachimbaji wadogo katika utafutaji na uchimbaji wa madini. Aidha, Wizara imeendelea kuwatafutia maeneo na kuwawezesha kupata ruzuku kwa ajili ya kuendeleza shughuli za madini kihalali na kwa tija. Katika kipindi hiki Serikali ilitenga maeneo 25 yenye jumla ya ukubwa wa hekta 204,713.8 na jumla ya leseni za uchimbaji mdogo (PML) 8,800 zilitolewa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliwasiliana na wamiliki wa Leseni Namba *PL6545/2010* yenye ukubwa wa kilomita za mraba 5.28 iliyopo katika kijiji cha Buziba huko Nyarugusu, Wilaya ya Geita ili waweze kuachia sehemu ya eneo lilotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Wamiliki wa leseni hiyo wameeleza kuwa tayari eneo hilo limeishaendelezwa na kufikia hatua ya kuanzisha mgodi. Hata hivyo wameonyesha uwezekano wa kupatikana eneo dogo nje ya mipaka ya eneo watakalo jenga mgodi, mazungumzo na kampuni hiyo bado yanaendelea. Pindi eneo litakapopatikana litafanyiwa tathmini ya mashapo ya dhahabu na GST na hatimaye litagawiwa kwa wachimbaji wadogo wa Nyarugusu.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, swali la msingi linataka kufahamu ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais itatekelezwa. Serikali inajibu kwa kusema wana kuwa wana mazungumzo na mmiliki wa Leseni Namba 6545. Swali, hayo majadiliano yatakamilika lini, kwa sababu Sheria ya Madini ya 2010 inasema ni nini kifanyike unapofika hatua ya kuanzisha mgodi kuhusiana na eneo ambalo lilikuwa katika *PL*?

Swali la pili, tunafahamu kuwa maeneo mengi katika nchi yetu yametolewa kwa wawekezaji wa ndani na nje, lakini baadhi yao wamehodhi maeneo haya. Mpango wa Serikali ukoje, kwa mujibu wa sheria kuhusu watu ambao wamekalia maeneo na hawayaendelezi na yako mengi sana? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE): Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi hilo hilo, nimeeleza juu ya jukumu la GST. Utaratibu tunaotumia sasa baada ya kukubaliana na yule mwekezaji

aliyekuwa amechukua eneo, ni lazima tuwatumie GST waende kuhakiki kwamba wale vijana tunaowapeleka kule wanakwenda kupata kitu chenye tija.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho sikueleza na ambacho ni jukumu la Kamishna wa Madini, ni kwamba, jitihada zimeshafikia hatua nzuri, wale vijana wa Rwamgasa watapata; na Mheshimiwa Bukwimba nilishamueleza wakati wa bajeti ya Nishati kwamba, kilio chake kiwe kidogo, umeipigania sana Rwamgasa na Rwamgasa wanapata na hilo suala ninalifuatilia pamoja na Mheshimiwa Bukwimba; na juzi wakati nakwenda Kagera watu wa Geita walinizuia niliwaambia maneno hayohayo; na Mheshimiwa Kitwanga analifuatilia kwa karibu.

Swali la pili, watu wanaohodhi maeneo; mkisikia kelele za Wizara ya Nishati watu wanashambuliwa ni wale wanaohodhi maeneo ndiyo wanashambulia watendaji na viongozi wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Waziri wangu aliishazungumza hapa kwamba, ameongeza kodi kusudi wale ma-speculators wanaohodhi waweze kuachia. Tunapambana nao na tumetoa maelekezo kwa Kamishna kwamba, wale wanaohodhi ni lazima wafutiliwe na tunatengeneza utaratibu ambao mtu atakuwa anapewa eneo sasa katika kipindi maalumu na baada ya hapo tunamwambia ondoka. Kazi ni kubwa lakini inafanyika.

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Busanda ni sawasawa na tatizo lililopo Ruangwa Mkoani Lindi. Mkoani Lindi kuna wachimbaji wadogowadogo wengi wa *Gypsum*, *Green Tourmaline* na Dhahabu, lakini, wachimbaji hawa sijaona hata siku moja wanapimiwa maeneo au wanapewa ruzuku kama wanavyopewa ruzuku maeneo mengine.

Naomba tafadhali, Serikali iangalie Kusini, Ruangwa, kuwapimia maeneo wachimbaji hawa wadogowadogo ili na wao waweze kujikimu na maisha.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sasa Serikali ituambie, ni lini watakuja Ruangwa kuangalia suala zima la wachimbaji wadogowadogo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE): Mheshimiwa Spika, kuna mambo mawili; usimamiaji wa wachimbaji wadogo katika Mikoa ya Kusini, ninavyojua usimamiaji unafanyika. Natoa maelekezo kwa Kamishna anayehusika kwa Kanda ya Kusini alete taarifa kabla sijasimama hapa tena kujibu swali linalokuja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ruzuku zinazotoka, nasisitiza kuna ruzuku itatoka kwa wachimbaji wadogo kabla hatujamaliza Bunge hili. Natoa maelekezo kwa wale wanaohusika, ni lazima ugawaji wa ruzuku usambae Tanzania sawia Kusini, Kaskazini, Mashariki na pande zote, tuhakikishe kote wamepata na tutatangaza kwenye gazeti kuonyesha usambazaji uliofanyika. Mheshimiwa Waziri anasimamia hilo na Mheshimiwa Kitwanga anasimamia hilo.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo na Chakula, anayeuliza swali ni Mheshimiwa Moshi Kakoso, swali hilo litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Issa Yahya.

Na. 230

Tatizo la Soko la Zao la Tumbaku

MHE. YAHYA KASSIM ISSA (K.n.y. MHE MOSHI S. KAKOSO) aliuliza:-

Zao la tumbaku limeshuka bei kwenye Soko la Dunia wakati wakulima wa zao hilo wakiwa wamezalisha tumbaku kwa wingi kupitia hamasa iliyotolewa na Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Edward Lowassa na Waziri Mkuu wa sasa Mheshimiwa Mizengo Pinda.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwafidia hasara waliyopata wakulima wa zao hilo nchini?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Suleiman Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bei ya tumbaku katika soko la Dunia imekuwa ikibadilika mara kwa mara kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ushindani wa uzalishaji na ubora wa tumbaku wa nchi zinazozalisha tumbaku duniani. Aidha, udhibiti wa bidhaa za tumbaku na matumizi yake unaofanywa na Shirika la Afya Duniani kupitia kampeni ya *Framework Convention on Tobacco Council* umesababisha pia kupunguza kwa matumizi ya bidhaa za tumbaku na hivyo kuathiri bei ya tumbaku kwa wakulima nchini, katika kuongeza uzalishaji na ubora wa tumbaku inayozalishwa nchini ili kuongeza bei kwa wakulima Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku itaendelea kuwafundisha wakulima kanuni za kilimo bora cha tumbaku. Lengo la mafunzo hayo ni kuongeza ufanisi na tija katikuzalishaji na ubora wa tumbaku ili kukidhi viwango vya ushindani katika Soko la Dunia na hivyo kuongeza bei kwa wakulima wa tumbaku nchini. Aidha,

Serikali itaendelea kutafuta masoko ya tumbaku katika nchi mbalimbali ili kuwezesha wakulima kuuza tumbaku kwa bei nzuri na hivyo kupata faida.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya kupanda na kushuka kwa bei za mazao ya biashara katika Soko la Dunia ikiwemo zao la tumbaku, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa mazao husika inaandaa utaratibu wa kuanzisha Mfuko Maalumu wa kufidia bei ya mazao (*price stabilization fund*) kwa ajili ya kusaidia wakulima pindi bei ya mazao inaposhuka katika Soko la Dunia.

Mheshimiwa Spika, waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya kutunga sheria ya kuanzisha Mfuko wa kufidia bei za mazao umewasilishwa katika ngazi za juu kwa maamuzi. Aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika ujenzi wa viwanda vya kutengeneza sigara ili kuongeza thamani ya zao la tumbaku badala ya kuuza tumbaku iliyosindikwa kidogo (*semi procesed*).

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ni muda gani Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku itatoa mafunzo hayo kwa wakulima?

Pili, wakati udhibiti wa bidhaa za tumbaku na matumizi yake unafanywa na Shirika la Afya Duniani; je unafikiria hata wakulima wakipewa mafunzo hayo, bei ya tumbaku inaweza kupanda?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, suala la mafunzo kwa wakulima ni endelevu, tunachokifanya hapa ni kutilia mkazo zaidi ili wananchi wahakikishe kwamba wanazielewa kanuni bora zaidi za uzalishaji wa tumbaku na hivyo hili jambo linafanyika mara kwa mara. Tunachokifanya sasa hivi ni kutilia mkazo zaidi kwa sababu inaonekana kama vile wakulima wakati fulani wanajisahau na kubaki wanazalisha tumbaku bila kuzingatia taratibu au kanuni zinazohusu zao lenyewe la tumbaku.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kama mafunzo haya yatafanywa na wakulima wakazingatia kwa ufanisi, bei hizi zinaweza zikapanda kwa sababu ubora ndiyo unao-*determine* bei ya tumbaku. Kwa hiyo, kama wakulima wakizingatia maelekezo ya uzalishaji kwa viwango vinavyokubalika na kuzingatia kanuni, tuna uhakika hata bei ya tumbaku pia au ni sababu mojawapo ambayo itasababisha kupanda kwa bei ya tumbaku.

SPIKA: Mheshimiwa Vita Kawawa, sijui bado ni Mwenyekiti wa Bodi ile!

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenye, ahsante. Na-*declare interest*, mimi bado ni Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bei ya mwaka 2014/2015, madaraja mengi zaidi ambayo yalikuwa yanamsadia mkulima yalishuka bei. Kwa mfano, bei ilishuka kwa 5% lakini madaraja ya kati yalishuka kwa 40%.

Mheshimiwa Spika, lakini wadau tumekaa na kusema kwamba mwaka huu 2015/2016 bei ibadilike na ijengwe tena kwa aina ambayo itamnufaisha mkulima. Sasa tulikuwa tunaiuliza Serikali, Wizara ya Kilimo iko tayari kutuunga mkono katika msimamo wa wadau na hasa wakulima kwamba bei mwaka huu ijengwe kulingana na gharama za mkulima na faida ipatikane kwa mkulima?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku nchini kwamba, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika iko tayari sana sana kushirikiana na Bodi yake. Inaweza ikawa ni ajabu sana Serikali ambayo imeunda Bodi hiyo halafu ikashindwa kupokea maoni ya Bodi, kwa sababu maoni hayo kwa kweli yanalenga kumsadia mkulima.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nimthibitishie kwamba, wale wanunuzi wakorofi na sisi hatutakubaliana nao. Tunajua analolisema, kampuni ya TLTC ndiyo ilikuwa ina tatizo hilo kubwa. Kwa hiyo, tumesema kwamba tutahakikisha tunayabana haya makampuni ili yakubaliane na maamuzi yanayofanywa na mteuzi wa Serikali au wa Bodi, maana walikuwa wanakataa hatua hizo. Kwa hiyo, sasa hivi tutahakikisha kwamba maamuzi yatakayofanywa na mteuzi wa Serikali yanazingatiwa ili wakulima waweze kupata bei nzuri zaidi.

SPIKA: Naomba tuendelee na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa atauliza swali linalofuata, kwa niaba yake, Mheshimiwa Mangungu.

Na. 231

Unywaji wa Maji ya Bomba Bila ya Kuchemsha

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. MARIA I. HEWA) aliuliza:-

Je, ni lini wananchi wataruhusiwa kunywa maji ya bomba moja kwa moja bila ya kuchemsha?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa kama ifuatavyo:-

Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inatekeleza miradi ya maji nchi nzima kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama. Maji safi na salama ni yale ambayo yanapitia hatua zote za kusafisha na kutibu, hivyo huduma ya usambazaji maji mijini na vijijini inahusisha ujenzi wa miradi yenye miundombinu ya kusafisha na kutibu maji kutegemea na aina ya chanzo na ubora wa maji hayo.

Mheshimiwa Spika, maji huhakikiwa ubora wake kabla na baada ya kusambazwa ili kuhakikisha usalama wake unakuwa endelevu. Hata hivyo, ushauri wa kuchemsha maji ya kunywa ni tahadhari endapo uchafuzi utajitokeza kwenye mifumo ya usambazaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za upatikanaji wa maji safi na salama kwa kufanya maboresho ya mitambo ya maji na ujenzi wa miradi mipya ya maji mijini na vijijini. Katika utekelezaji wa miradi hiyo, suala la miundombinu ya kutibu maji limepewa kipaumbele.

Aidha, Serikali inaandaa mpango unaohusisha utaratibu wa usafi na usalama wa maji kuanzia kwenye chanzo hadi kwa mtumiaji. Mojawapo ya matokeo ya mpango huu ni kupunguza gharama kubwa ya kusafisha na kutibu maji ya kunywa. Mpango huu unahusisha taasisi zote za usambazaji wa maji ili kutoa uhakika wa maji yanayotumika kuwa ni safi na salama. Hivyo, jitihada hizi zikifanikiwa maji ya bomba yataweza kunywewa bila ya kuchemshwa.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nataka kujua ni nini jitihada za Serikali kwenye kuhakikisha kwamba uchafuzi wa maji hasa kwenye vyanzo vyake yanakwenda sambamba na mradi mkubwa wa maji ambao unapeleka maji katika Mikoa ya Shinyanga, Geita pamoja na Tabora. Ni nini mpango wa Serikali kusimamia mpango huo?

La pili, tunao mradi mkubwa wa maji ambao unatoka eneo la Mingumbi kwenda Miteja, Tingi pamoja na eneo la Somanga, Waziri ameishalitembelea. Ni nini kasi ya Serikali katika kusukuma mradi huu uweze kutoa tija na manufaa kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, la kwanza, Serikali inafanya kila jitihada kwa kuwashirikisha wananchi maeneo hayo ambayo kuna vyanzo vya maji na siyo tu Ziwa Victoria, lakini na maeneo yote ambayo kunakuwa na vyanzo vya maji ili kuona kwamba shughuli za kijamii hazifanyiki, lakini pia kuona kwamba maji yale hayachafuliwi ili tuweze kuyapata yakiwa safi na salama. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuendeleo kuwahamasisha wananchi kutokufanya kazi za kijamii katika vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, la pili; ni kweli nimefika katika jimbo lake na nimeona mradi ambao ameutaja wa Mingumbi, Miteja na Chumo. Niseme tu kwamba, bajeti imeshapitishwa, sisi tutakapopata fedha, miradi hii itaendelea kujenga miundombinu.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, swali la msingi la Mama yangu Mheshimiwa Maria Hewa, alipenda kujua ni lini wananchi wa Tanzania watakuonywa maji ya bomba moja kwa moja. Kwa kuwa Tanzania kwa zaidi ya 80% wananchi wanakunywa maji ambayo siyo tu safi na salama, ni maji machafu yenye viluilui. Ningependa Mheshimiwa Naibu Waziri ajibu swali la msingi kwamba ni lini, ni miaka mingapi itachukua kwa Watanzania kuunganishwa kwa maji ya bomba ambayo tutakunywa moja kwa moja kama tunavyoenda nchi za nje tunashudia wenzetu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi nimesema hatua mbalimbali zinazopitia kuona kwamba wananchi wanapata maji safi na salama. Lakini pia tumeeleza mikakati inayofanyika, tunataka kufanya mikakati kwamba maji yote tutakayoyapata na baadaye tufike wananchi wote wanywe maji ambayo hayapitii katika process ambayo inafanyika sasa, ambayo ni gharama. Kwa hiyo, siyo lini tu ni kwamba mpango huu umeanza, ni mpango mkakati, utakapokuwa umekamilika tutawatangazia wananchi wote.

SPIKA: Kwa sababu ya muda, tuendeleo na swali linalofuata. Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, kwa niaba yake, Mheshimiwa Abdulsalaam.

Na.232

Mradi wa Maji wa Masoko, Wilayani Rungwe

MHE. ABDULSALAAM SELEMANI AMER (K.n.y. PROF. DAVID H. MWAKYUSA)
aliuliza:-

Mradi wa maji wa Masoko Wilayani Rungwe uliotarajiwa kunufaisha wananchi wa Vijiji 15 ulisainiwa mwaka 2009 na ulitegemewa kukamilika na kukabidhiwa kwa wananchi mwezi Agosti, 2011, lakini hadi leo hakuna hata kaya moja iliyopata maji ya mradi huo.

Je, Serikali ina nia ya kweli ya kuwapatia wananchi hao maji hasa ikizingatiwa kuwa miradi mingi mipya imeanzishwa humu humu nchini na kukamilika wakati mradi wa Masoko ambao ungekamilika miaka minne iliyopita bado unawekwa kando?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Masoko ni miongoni mwa miradi mikubwa ya maji inayotekelezwa Wilayani Rungwe ambayo inagharamiwa na Serikali kwa asilimia 100%. Ndani ya mradi huu vipo vyanzo vitatu vya maji ambavyo ni Mbaka, Kigange na Ndululunga vinavyohudumia kata tatu za Masoko, Masukulu na Ikama zenye vijiji 15 vya Halmashauri ya Rungwe.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina nia ya dhati ya kuendeleza na kukamilisha miradi yote nchini ukiwemo mradi wa Masoko. Utekelezaji wa mradi huo ulisimama kutokana na mgogoro uliojitokeza kati ya halmashauri na mkandarasi na kupelekea mkataba kuvunjwa. Kwa sasa Wizara imeagiza Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kuanza utaratibu wa kumpata mkandarasi mwingine wa kukamilisha kazi zilizobaki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 kiasi cha shilingi bilioni 1.7 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi.

MHE. ABDUSALAAM SELEMANI AMER: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo la suala la mkandarasi kama ilivyotokea Wilaya ya Rungwe ni tatizo la nchi nzima. Kuna baadhi ya wakandarasi wanakuwa hawana uwezo au wababaishaji. Je, Serikali kama Wizara itachukua hatua gani ya kuwadhhibiti wakandarasi kama hawa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; tatizo la maji ni sehemu nyingi, kwa mfano katika Mji wangu Mdogo wa Mikumi mradi wa maji umeishakamilika kwa asilimia 80. Mji Mdogo wa Mikumi sasa hivi unakua, una wakazi zaidi ya 10,000. Je, ni lini Serikali itatoa hizo pesa ili maji yatoke kuwasaidia wananchi wa Mji Mdogo wa Mikumi hasa tatizo la *pump* na umeme tu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, suala la wakandarasi kukosa sifa na uwezo limejitokeza katika maeneo mbalimbali, lakini, niwaombe Mheshimiwa Wabunge, sisi ni sehemu ya Kamati za Fedha za Halmashauri, na kwamba wakandarasi hawa sasa siyo Wizara ya Maji inawaajiri, wanaajiriwa na Halmashauri zetu. Kwa hiyo, tuangalie vigezo na kuangalia wakandarasi wazuri ambao wanaweza wakafanya kazi hizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mradi wa Maji Mikumi; kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia mara kwa mara na mimi mwenyewe nimefika hapo. Ni kweli anachosema, mradi umebaki kidogo.

Mkandarasi kwa sasa anadai fedha, na kama tulivyoahidiwa, tukipata fedha, tutamlipa na mradi ule ukamilike.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba lini fedha zile ambazo Mheshimiwa Waziri wa Fedha, alituahidi hapa kwamba atazilipa hapa kabla ya tarehe 30 zitaanza kugawiwa ili mradi mkubwa wa Chiwambo, Ukululu na Chipinga uweze kuanza kazi?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda tu kutoa maelezo kuhusiana na fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Serikali iko palepale, na kwamba sasa hivi tupo katika *process* ya kuzi-*mobilize* na once tukizipata tutazipeleka Wizara ya Maji kwa ajili ya kwenda kufanya kazi ambayo imekusudiwa. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, ahadi ya Serikali bado iko pale pale.

Na. 233

VETA Kujenga Hoteli na Kiwanda cha Minofu ya Samaki Lindi

MHE. SALUM K. BARWANY aliuliza:-

Serikali imejenga Chuo cha VETA Lindi na pia ilikuwa na mpango wa kujenga hoteli kwa lengo la kutoa mafunzo kwa vijana wetu:-

- (a) Je, Serikali imefika wapi kwa suala la ujenzi wa hoteli hiyo?
- (b) Je, VETA wana mpango gani wa kuwa na kiwanda cha minofu ya samaki kama vile cha Dodoma?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfani Barwany, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa Hoteli ya Mafunzo ni kutengwa kwa eneo la Mitwelo lenye ukubwa wa ekari 32.75 ambapo VETA imeishalipa gharama za fidia kwa Manispaa ya Lindi. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti taratibu za ujenzi huo bado hazijaanza kwa vile Serikali imejikita zaidi katika kutafuta fedha za ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya ambazo hazina vyuo hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, wakati wa kuanzisha Chuo cha VETA Lindi, Mamlaka ilifanya uchambuzi wa stadi zinazohitajika, ambapo stadi za usindikaji wa minofu ya samaki haikujitokeza kwa kipaumbele kwa wakati huo. Kwa kuwa lengo la VETA ni kutoa mafunzo yanayoendana na soko la ajira, Serikali katika mwaka 2015 itaanza kutoa mafunzo ya uandaaji wa minofu ya samaki kwa utaratibu wa kozi fupi kwa walengwa.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ifahamike kwamba Lindi ni Mkoa kati ya jumla ya mikoa katika awamu ya kwanza ya ujenzi wa vyuo vya VETA. Kwa maana hiyo sasa, Lindi kulihitajika kukamilisha *package* nzima ya vyuo hivyo, ikiwepo ujenzi wa hoteli. Mheshimiwa Waziri haoni kwamba awamu ile ya kwanza kama mikoa, ujenzi wa chuo cha VETA Lindi haujakamilika kwa mujibu wa *package* yake?

Swali la pili, Serikali tayari imeishatoa Azimio au tamko rasmi kwamba kuna miji mitatu katika nchi yetu; Kigamboni – Dar es Salaam, Lindi pamoja na Mtwara! Hiyo Miji ni *new city* (miji mipya) ambayo kwa ujio wa gesi itakuwa ni miji mashuhuri duniani. Hivyo, tunatarajia kupata wageni kutoka katika maeneo mbalimbali ndani ya nchi na nje.

Je, hatuoni kuna hitaji kubwa sasa la watu wenye taaluma ya hoteli kwa ajili ya kuwapokea wageni hao?

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa sasa, badala ya kufikiria ujenzi wa vyuo vya VETA katika wilaya mbalimbali kwa umuhimu wa Mji wa Lindi kwa sasa?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, moja kuhusu *package* kukamilika; *package* ambayo tulikuwa nayo ni muhimu kwa Lindi, ni kukamilisha Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa Mkoa wa Lindi, ambapo kwa ushirikiano na Serikali ya Korea tumejenga chuo kizuri kikubwa ambacho sasa kinatoa mafunzo wa wana-Lindi; na kwa maana hiyo tutaendelea na *phases* zingine, kadri ya upatikanaji wa pesa tutaweza kufanya na hayo ambayo wana-Lindi wanayahitaji na hasa kwa vile tayari kiwanja kimeishapatikana.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa swali la pili, msisitizo mkubwa uliopo sasa hivi kwa Serikali ni kukifanya Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi Lindi kama vile cha Mtwara, kuwa ni vyuo mahiri ambavyo vitaweza kuhudumia sekta ya mafuta na

gesi kwa Kusini. Kwa hiyo, fani ambazo tunaziongezea uwezo hivi sasa kwa Lindi na Mtwara ni zile ambazo zitaweza kuhudumia uchumi huu wa gesi na mafuta kwa Lindi na Mtwara.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mkinga ni miongoni mwa Wilaya 20 zilizoko kwenye orodha ya mwanzo ya kujengewa chuo vya VETA. Serikali iliahidi ndani ya Bunge hili kwamba mara baada ya kukamilisha ujenzi wa chuo kule Kilindi utafuatia ujenzi katika Wilaya ya Mkinga. Ni lini utekelezaji huo utafanyika?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa ujenzi wa Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi, tuna orodha ya Wilaya 43. Hata hivyo, kama nilivyojibu swali hili awali na mara kadhaa, tatizo kubwa ambalo Serikali imepambana nalo ni ukosekanaji wa pesa za kutosha kuweza kujenga vyuo hivi kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa, Kilindi ambayo imepangwa pamoja na Wilaya zingine tano, ikiwemo Ludewa, Chunya, Ukerewe, tupo katika maandalizi ya kukamilisha vyuo hivi na sasa hivi wakandarasi karibu wataingia katika baadhi ya Wilaya kama vile Namtumbo. Lakini, kabla hatujakimilisha hayo, hatutoweza kwenda kwenye vyuo vingine, tutegemea kwamba kadri muda unavyokwenda pengine katika awamu inayokuja, tutaweza kufanya kazi nzuri zaidi katika kundi hilo la kwanza la Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi.

SPIKA: Maswali yamekwisha na muda pia umepita. Naomba nitambue baadhi ya wageni ambao wapo humu ndani, ambao nimeletewa orodha yao hapa! Nina wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni 40 wa Mheshimiwa Dkt, Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) kutoka Jimbo la Hanang ambao ni wachezaji wa mpira wa miguu, wakiongozwa na Mheshimiwa Charles Yona, Diwani wa Kata ya Gendabi. Naomba hao wote wasimame walipo! Ahsante sana karibuni sana.

Tunao wageni 35 wa Mheshimiwa Ester Matiko ambao ni wachezaji 15 wa *Matiko New Vision Sports Academy*, ambao wanachuana na timu ya *Bunge Sports Club* na timu ya *Veterinary*, wakiongozwa na ndugu Mwita Mwase. Hawa pia naomba wasimame kama wamepata nafasi! Ahsante sana.

Yupo Ndugu Makame Issa (Muamuzi) ambaye ni kijana mdogo. Enhe, huyo kijana mdogo asimame! Yuko katikati yao. Kuna ndugu Lucas Jeremia (Kocha).

Viongozi wa Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA) na viongozi wa Baraza la Vijana (BAVICHA) wakiongozwa na Mzee Jacob Kinyanga kutoka Wilaya ya Tarime. Hawa nao wote wasimame huko waliko. Halafu tuna ndugu Martin na ndugu Jacob (Makatibu wa Mbunge). Wasimamee, ahsante sana! (Makofi)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Hasnain Murji ambao ni wanafunzi 33 na walimu wao kutoka Shule ya Msingi Chuno, Mtwara. Naomba wasimame! Msome kwa bidii wameshawaambieni vyuo vya gesi vipo huko huko basi na ninyi mkasome.

Tuna wageni wa Mheshimiwa John Paul Lwanji ambao ni wanachuo 45 kutoka Chuo cha Biblia na Maendeleo Sanjaranda, Ifigi, wakiongozwa na ndugu John Tuu, Mkuu wa Chuo. Naomba wasimame kama wamepata nafasi! Ahsanteni sana. Msome kwa bidii!

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Salum Barwany ambaye ni Ndugu Abna Okero kutoka *Tanganyika Christian Refugee Services (TCRS)*. Ahsante sana karibu na pole na kazi kubwa.

Tuna wageni ambao wamekuja Bungeni kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 71 kutoka Chuo Kikuu cha St. Johnes Dodoma. Naomba wasimame kama wamepata nafasi! Karibuni majirani zetu, someni kwa bidii. Wanafunzi 41 na walimu 7 kutoka *St. Joseph Millennium Primary School Dar es Salaam*; na hao wasimame kama walipata nafasi. Karibuni sana nanyi msome kwa bidii.

Tunaye Bi. Evelyne Maziku, yupo kwa ajili ya kutembelea Bunge na ameambatana na watoto wake wawili kutoka Dodoma. Ahsanteni sana. Hao Wabunge wa kesho! Karibu sana.

Shughuli za kazi: Mwenyeti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Anna Abdallah, anaomba awatangazie Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kuwa, leo tarehe 19 sasa saba mchana watakuwa na kikao chao katika ukumbi namba 229.

Mwisho wa matangazo. Katibu!

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2014 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

na

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Ahsante. Ni kusudio langu leo kwamba wale wachangiaji wote waliobaki wanamalizika leo. Kwa hiyo, naanza kumuita Mheshimiwa Bahati Abeid, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Hassan, Mheshimiwa Masoud Salim na Mheshimiwa Ester Matiko ajiandae!

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi hii leo ili niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na afya yangu, leo ningependa nichangie kwa maandishi, lakini kwa kuwa nimepata nafasi hii, naomba nichangie machache, japo nina waraka nimeshauandaa, nitaupeleka kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Fedha na Manaibu Waziri kwa hotuba hii nzuri ambayo ametuletea kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu, lakini pia napenda nimpongeze sana Waziri wa Mipango.

Mheshimiwa Spika, nianze kama walivyotangulia kusema wenzangu kwamba, mafuta kwa kweli yakipanda kila kitu kinapanda. Hili ni jambo ambalo halipingiki, ni jambo ambalo lililo wazi. Ni lazima tuangalie kwenye mafuta, wanaoumia ni watumiaji wa mwisho, wanaoumia ni wananchi.

Mheshimiwa Spika, nampenda sana dada yangu Waziri wa Fedha, lakini kwenye suala la mafuta sipo pamoja naye na wala simuungi mkono kwenye suala hili la mafuta, naomba sana aliondoe kabisa. Wananchi maisha yamepanda, dola imepanda ipo juu! Kila kitu kimepanda, na leo tunawaongezea mzigo huu wa mafuta, hili haliwezekani!

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, niende kwenye suala zima na hili ndilo ambalo nimeliandikia kwa upeo mkubwa sana, na nimelifanyia utafiti mkubwa sana, suala la kuajiri na kupandisha mishahara na vyeo kwa ajili ya wahasibu.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kukaa na dada yangu Saada hapa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha nikamueleza kwamba suala hili la upandishaji wa vyeo kwa wahasibu wa Wizara ya Fedha wanafaidika, lakini wahasibu wa Wizara nyingine zote wananyanyasika kwa kupandishwa vyeo lakini pia kwa kuangalia mishahara yao. Ukiangalia leo kama atajiriwa mhasibu wa diploma, basi anafanana mshahara wake na yule ambaye amejiriwa tangu miaka kumi na tano iliyopita, ambaye hana diploma lakini ana digrii mshahara wake unafanana.

Mheshimiwa Spika, huu ni unyanyasaji, ni unyanyasaji mkubwa! Mimi najua wahasibu wote wapo chini ya Wizara ya Fedha, ni lazima waangaliwe kwa makini maslahi yao lakini na upandishwaji vyeo. Haiwezekani uzoefu alionao mhasibu ambaye ana digrii, ukamlinganisha mshahara wake na wa diploma, haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, lakini pia wana kigezo wanachokitumia, mpaka uwe na CPA ndipo upandishwe cheo! Mimi naomba mipango yao hii waiangalie kwa makini. Nimewaandikia pia kwa makini kwenye *paper* yangu hii; na Waziri wa Fedha atakapokuja lazima atupe majibu ya kina kwa sababu kuna unyanyasaji mkubwa na wafanyakazi hawa ni wengi wanaonyanyasika na wanaodhulumiwa kwenye maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, nikiangalia wale walio vijijini, wanazidi kunyanyasika, lakini hata wahasibu waliopo Ofisi ya Bunge. Mimi nina mfano tosha, tulikuwa na mhudumu wa Bunge, ndani ya Bunge baadaye akajiendeleza akapata nafasi ya uhasibu, mimi nimeingia miaka kumi nan ne iliyopita ndani ya Bunge, anapata sawasawa na wale wahasibu ambao nimewakuta. Hii siyo sawa! Ni lazima eneo hili liangaliwe kwa kina, tena kwa kina kikubwa!

Mheshimiwa Spika, pia niseme kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya LAAC, natembea Halmashauri zote.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuna miradi mingi sana imeanzishwa lakini tunashindwa kuimalizia. Ni lazima tuwe na miradi michache ambayo tunaweza kuitekeleza kwa umakini mkubwa. Ipo miradi ambayo imeanzishwa na sasa hivi imeshavurugika kutokana na pesa kutopelekwa kwa wakati lakini pia kutokupelekwa kabisa. Ni lazima miradi tutakayoianza imalizike. Kama hatuna uwezo wa kuimaliza, basi tusiianze maana yake zile ni pesa za wananchi, zinapotea bila kuangalia.

Mheshimiwa Spika, lingine ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inapewa bajeti ndogo na ukiangalia Wizara hii inapeleka fedha ndani ya Halmashauri zetu kule katika vijiji vyetu. Fedha hizi tunategemea wanawake wengi wakopeshwe waondokane na umaskini.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri tumewaambia mapato yao ya ndani watoe asilimia tano kwa vijana na asilimia tano kwa akinamama, lakini Halmashauri nyingi hazitekelezi. Kwa hiyo, tunategemea sana Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto wapeleke fedha zile kwa akina mama ili angalau akinamama waweze kukopa na kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, nitasema kidogo tu kwa afya yangu leo, lakini nina waraka hapa nimeuandaa, nitauwasilisha kwa Waziri wa Wizara ya Fedha ili aurfanyie kazi. Atakapokuja kutoa majibu naomba sana aligusie suala hili kwa sababu linagusa watu wengi sana; wafanyakazi wengi wananyanyasika. Aligusie kwa kina na awaonee huruma.

Hivi vigezo vyao walivyoviweka, haiwezekani kwamba kila baada ya miaka mitano sisi tuna mipango mipya lakini wao wanaendelea na manyanyaso haya wanayoyapata.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mussa Hassan, atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Salim.

MHE. MUSSA HASSAN MUSSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nikawa mmoja wa wachangiaji wa hotuba iliyo mbele yetu. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah-Wataalah* kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuchukua muda mfupi kusema na jamii ambayo inanisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa ujasiri na weledi wako wa kuendesha shughuli za Bunge ukisaidiwa na wasaidizi wako wakiwemo Katibu wa Bunge na Maofisa wengine.

Mheshimiwa Spika, nashangaa, kwa mujibu wa weledi wako, ujuzi wako, sijakusikia bado na wewe kujiunga kwenye kinyang'anyiro! *(Kicheko/Makofi)*

SPIKA: Hukuniona jana nilikwenda, lakini nikakosea njia, nikaenda kwenye Bima ya Afya! *(Kicheko/Makofi)*

MHE. MUSSA HASSAN MUSSA: Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba sasa niwashukuru Wapiga kura wangu wa Jimbo la Amani kwa kuniamini na kunipa dhamana ya kuwakilisha katika chombo hiki. Ni imani yangu kwamba kipindi kifupi kijacho wataendelea kunichagua tena ili kushirikiana nao katika kuleta maendeleo katika Jimbo letu na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya maeneo hayo, sasa naomba nijielekeze katika kuchangia hotuba tuliyonayo ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pamoja na kwamba imetanguliwa na Waziri wa Mipango.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba kupanga ni kuchagua. Nataka kuipongeza Serikali kwa umahiri ambao imetupangia vipaumbele mbalimbali ili kuleta maendeleo katika nchi yetu. Pamoja na mambo mazuri yaliyopangwa, kawaida viumbe wanasema 'aso kasoro hakuna.' Lakini kitu ambacho kinasikitisha ni kuona umoja wetu hapa, tunaoitwa Wabunge, tuna kazi moja tu kuishauri na kuisimamia Serikali kuhakikisha kwamba inaleta maendeleo kwa wananchi au kwa nchi yetu kwa ujumla. Sasa inanipa taabu kuona kuna baadhi ya Wabunge badala ya kushirikiana, wanajaribu kutoa kasoro kwa vile ni haki yao, lakini watumie vizuri haki kwa sababu haki unapoitumia ni lazima uangalie na wajibu, au wajibu unaenda sambamba na haki.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kinaonekana kwa wenzetu hawa, ama ni tamaa ya fisi kuona mkono unatembea labda utakatika, lakini hizi ni ndoto za Alinacha. Siyo rahisi kabisa kwa utitiri huu wa Vyama sasa kuona kwamba umefika wakati wa kusema na wao wana haki ya kushika dola. Siyo rahisi! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali hii inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi imefanya mambo makubwa sana. Hapo wanapojihisi kwamba wapo kwenye boti au mashua inaelea, basi wahakikishe kwamba hiyo mashua imeundwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne ina kila haki ya kutembea kifua mbele kwa mambo mengi mazuri ambayo imeyafanya. Tukiangalia miundombinu, sasa hapana sehemu ambayo haifikiki na inafikika kwa muda mfupi tu. Hali kadhalika, Serikali hii imewezesha sasa kwa wanawake kuzungumza hadi kusema kwamba tunataka asilimia hamsini hamsini. Haya ni maendeleo! Siyo kitu ambacho kimeibuka tu! Hii ni mipango madhubuti ambayo imepangwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Kikwete.

Mheshimiwa Spika, mbali na hayo, tuangalie nchi yetu sasa ilivyokuwa na weledi, umahiri, vijana wasomi na maendeleo ya teknolojia haya nayo yanatokana na mfumo mzuri wa elimu ambao nao pia umepangwa na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi. Kama hilo halitoshi, najaribu kwenda ukurasa wa tano.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ukurasa wa tano kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, inasema Serikali imepanga kwenye bajeti hii kupunguza kodi hasa kwa vifaa vya uvuvi, pembejeo na vinginevyo ambavyo

vinamsaidia mwananchi kupunguza ukali wa maisha ya kila siku. Haya nayo ni mambo ya kuangalia na mambo ya kuyapigia mfano katika uendeshaji wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitoka hapo, ukiangalia ukurasa wa 37 bajeti hii inaelekeza kusema kwamba misingi ya bajeti hii ni kuhakikisha inadumisha amani, utulivu na usalama wa nchi hii. Tanzania inatajwa kila pembe ya dunia kwamba ni nchi tulivu, nchi ambayo imetawaliwa na amani. *Item* hizi mbili zinatoshleza kabisa kusema kwamba ni nchi ambayo tunaweza tukapata maendeleo. Nataka nitoe Indha kwa wale watu ambao wameweka masikio wazi kusikiliza baadhi ya wachangiaji au wasemaji katika vyombo hivi kusema nchi hii haina maendeleo, sisi tutakamata dola, lakini kitu cha kwanza cha msingi ni amani. Bila amani hakuna maendeleo yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuangalie, Chama cha Mapinduzi katika uhai wake, lini nchi hii imeonekana kwamba labda imetetereka kwa upande wa amani? Ndani ya nchi hii baada ya kupata fursa ya kuwa na Vyama vingi, sasa tuangalie mienendo ya Vyama. Utasikia maandamano, lakini maandamano hayo hayatamalizika; kuna huyu kapigwa, huyu kafanyaje, hii yote ni kujaribu kuleta maendeleo lakini kwa njia ya vurugu. Hatuna nafasi ya kuwapa uongozi watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba ndugu yangu Waziri wa Fedha aangalie uwezekano wa kuhakikisha kwamba fedha iliyotengwa kwenye bajeti inafika katika maeneo yaliyopangwa kwa wakati. Kuna vitu ambavyo vinavunja moyo kiasi fulani; kwa mfano, tumesikia hapa Waziri wa Mambo ya Ndani akijibu maswali mengi kuhusu namna gani uzembe na matukio tofauti yanatokea.

Mheshimiwa Spika, mathalan ninapoambiwa kwamba Kituo cha Polisi kimevamiwa na Polisi wanafanya jitihada za kuhakikisha kwamba wahusika wanatiwa mkononi na hatimaye kupelekwa kwenye vyombo vya sheria; lakini utalaam tulionao leo unanipa maswali kwamba inakuwaje kwenye Kituo cha Polisi tunashindwa kuweka *CCTV Camera*, tukaweza kumwona yule mhalifu ambaye anakwenda kuvamia kituo, wakati nyumba za watu binafsi zina uwezo wa kuwa na *Camera* kama hizo? Ni kitu cha ajabu sana! Sasa haya yote sidhani kwamba yanashindikana kufanyika lakini shida ni uwezesaji. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba sana uhakikishe fedha hii inakwenda kwa wakati na kuangalia vipaumbele katika utekelezaji wa malengo yetu haya.

Mheshimiwa Spika, kama hilo halitoshi, suala zima la utafiti ambao umefanyika karibuni, nchi yetu Tanzania inaonekana itakuwa ni nchi ya pili kuendelea kuwa nchi ya mwanzo ambayo itakuwa ina vijana wengi ambao hawana kazi katika Miji Mikuu kwa maana ya Jiji la Dar es Salaam. Hofu niliyokuwanayo, wakati Mji wa Dar es Salaam utakapofurika vijana ambao

hawana kazi, basi sehemu ya vijana hao wataangukia kwenye Kisiwa cha Zanzibar ama Kisiwa cha Pemba. Pale kwetu sisi tunasema kwamba Zanzibar ni njema, atakaye aje. Tunakaribisha! Hata hivyo, ni vema wakaja watu kwa misingi ya kuendeleza Muungano, kuudumisha na pia kuja kufanya kazi kuongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa misingi hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha ahakikishe kwamba mikopo ya vijana mashuleni na halikadhalika kuweza kutanua ajira, kuwawezesha vijana hawa ili kuweza kuwa na shughuli ambazo zinafanya wajitegemee katika maisha yao, tuondokane na msongamano wa vijana ambao hawana kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninataka niombe kwa nguvu zote, Serikali sasa tumo katika uandikishaji. Nashukuru sana na hapa pia nawapongeza wale watani wenzetu wa Vyama vya Siasa, wameonesha jitihada ya kushawishi wafuasi wao kujiandikisha. Naomba sana waoneshe jitihada hiyo pia kuelimisha namna na ustaarabu wa kwenda kupiga kura. Nchi yetu ni ya kidemokrasia; kila mmoja ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa, lakini kwenda pale kuna utaratibu maalum, hakuna sababu ya kwenda kwa vurugu. Shughuli hii tunawaachia wananchi. Wananchi ndio wana mamlaka ya kuchagua nani ni kiongozi bora na Chama gani kina haki au kina uwezo wa kupewa idhini ya kuongoza nchi hii. Suala la fujo, vurugu hazina nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana Viongozi wa vyombo vya Dola, hatuna nafasi katika kipindi hiki. Wengi wamesema na wanasema kwa nyakati tofauti kwamba mara hii tutaingia Ikulu, mara hii tutaingia Ikulu, mara hii tutaingia Ikulu, mara hii tuachieni sisi tuendeshe Ikulu. Tutavunja Muungano! Haya yanatoka wapi? Kuna filsofia moja ambayo mimi sielewi kama ina ukweli kiasi fulani. Inasema uwongo ukusema mara sabini, unakuwa ukweli. Hapana! Ukweli tuwaachie wananchi na masanduku ya kura. Siku ya tarehe 25 ikifika, wao ndio wanafanya maamuzi. Anayeingia Ikulu ataingia na atakamata hatamu za dola kuendesha nchi hii kwa ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nashukuru sana na ninarejea kuwaomba wanachama na wananchi wa Jimbo la Amani kuendelea kunipa imani kunichagua ili tuendeshe nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Masoud Salim!

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu *Sub-hanah-Wataalah*, kunijalia uzima na afya njema. Leo tupo katika siku ya pili ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani, mwezi

ambao una mambo mengi ya kufanya na kuwa karibu na Allah Subhanah-Wataalah kujua upungufu uliyopita, namna ya kujirekebisha na inshallah bin-lillah tufike lengo lililokusudiwa.

SPIKA: Nitakusikiliza kama umejirekebisha! (Kicheko)

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, nianze na suala zima la kuwapongeza kwanza Viongozi wangu Wakuu wa Kitaifa; Mwenyekiti wa CUF Taifa, Mheshimiwa Lipumba; Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Duni; Katibu Mkuu, Maalim Seif Sharif Hamad; na Viongozi wote. Pia nampongeza Kiongozi wangu wa Upinzani ndani ya Bunge hili na Mwenyekiti wa Bunge wa CUF pia yupo hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nianze na suala zima la nidhamu ya bajeti. Ni dhahiri kwamba muda wote ambao tumekuwa tukiongea, nidhamu ya bajeti hakuna. Sasa inaonekana kwamba Serikali wametia pamba za masikio. Tatizo hili ni kwamba, inakuwaje sisi tunapitisha bajeti lakini inafanya mambo yasiyostahili? Matumizi yanayofanyika ni makubwa kuliko sisi Waheshimiwa Wabunge tulivyopitisha? Ni nani aliyeidhinisha? Kwa nini Serikali itumie zaidi kuliko yale tuliyopitisha sisi Waheshimiwa Wabunge? Tatizo ni nini? Tabia hii mbaya ni lini mtaichacha?

Mheshimiwa Spika, tumesema mara nyingi juu ya tatizo hili kwamba kiwango cha fedha ambacho sisi Waheshimiwa Wabunge tunapitisha, ni vema Serikali ifuate. Nidhamu ya matumizi ya fedha; Bajeti ina nidhamu yake. Kwa hiyo, tuangalie mambo haya ya msingi.

Mheshimiwa Spika, katika hili naona kwamba nidhamu ya bajeti, bado Serikali haijawa makini kwenye kudhibiti wizi, ubadhilifu wa fedha na ufidadi. Mara nyingi tumekuwa tunatoa maelezo haya, lakini bado Serikali katika maelezo mbalimbali wanayotupa hapa majibu yao, haioneshi dhamira ya kweli kwamba kweli watakomesha wizi, watakomesha ubadhirifu, watapinga na ufidadi. Mimi napata mashaka juu ya hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo niongelee habari ya utegemezi. Mheshimiwa Saada Mkuya, tunaendelea kuwa na bajeti tegemezi kwa sababu matumizi yetu ya ndani ya kawaida ni makubwa kuliko mapato. Serikali inasema makusanyo yenu yanapungua. Tulishasema zamani, kuna vyanzo kadhaa vya mapato! Lakini tunapotoa ushauri wetu kupitia upande huu hasa Kambi ya Upinzani, sijui kwanini mna kigugumizi! Wananchi wanaona! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana basi dalili zinaonekana kwamba kweli sasa Upinzani kwa maana ya UKAWA mwaka 2015 watafanya kweli, kila dalili zinaonekana. Kwa sababu kila tunachosema; kwa mfano tumesema uwezo wa

vyanzo vingi vya mapato vipo. Siyo kama ninyi mfikiri, sisi tumeshafikiri! Tunawaambia ninyi, angalieni kwenye bahari kuu, angalieni kwenye migodi ya madini ambako kuna uzembe huko watu wanajichukulia wenyewe tu! Lakini tukawa tunasema aah, tupo katika michakato, tulieni kwanza. Tutaangalia haya mambo kidogo kidogo! Sasa hili nalo ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, namwambia Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba yale mapendekezo ambayo sisi tunapendekeza, basi ni vema hasa mwangalie. Mmeacha ulevi mwaka huu; mara hii walevi *alhamdulillah* mmeacha! Si haba! Mmeacha kuongeza fedha kwenye ulevi, sigara na pombe lakini mmekwenda kwenye mafuta ya taa, mmekwenda kwenye *diesel* na *petrol*.

Mheshimiwa Mbunge aliyepita, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid amesema, siyo muda mrefu, kwamba ukigusa *diesel* na *petrol* maana yake, kila kitu kitaongezeka. Nami kwa hili sikubaliani nalo hata siku moja! Hili liondolewe, haliwezekani! Hata sababu mliyotoa ya mafuta ya taa kwamba kuna moja, mbili, tatu, lakini pia mwangalie na vijijini! Kama lengo lenu mnasema namna ya kuchakachua na kudhibiti, lakini angalieni vijijini mtakavyoumiza watu kuhusu mafuta ya taa. Msiangalie hilo la kwenu peke yenu tu, mwangalie na mwananchi aliyepo kijijini, hili ni tatizo. Namwomba sana Waziri wa Fedha hili aliangalie.

Mheshimiwa Spika, katika jambo la pili, kuna deni la Taifa. Mwaka huu hili deni la Taifa hadi Machi ni trilioni 35, lakini Machi mwaka 2014 ilikuwa trilioni 30.6, ongezeko la 21%! Sasa hii kasi ya kuongezeka deni la Taifa ni kubwa kulikoni kasi ya kuongezeka pato la Taifa. Hili ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna historia ya kushindwa kulipa madeni. Tunayo historia hiyo, hatulipi madeni! Sasa kusema hii kauli kwamba hili deni ni himilivu, hiki ni kichekesho. Kwa sababu, hata deni la Mifuko ya Hifadhi, hapa hatulipi! Hili ni tatizo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaposhindwa kulipa madeni katika Mifuko ya Hifadhi, wanadai sana hawa; na kila siku wamekuwa wakilalamika; *PSPF* wanalalamika, *NSSF* wanalalamika! Bajeti kile tunachokusanya sasa, ni hali halisi ilivyo! Sasa mnajirekebisha kwa sababu ni karibu na uchaguzi tu! Wananchi si wanaona! Mtaona keshokutwa, tarehe 25 Oktoba, mtaona mziki wa UKAWA utakavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wananchi wanapata mori ikiwa kodi yao wanaiona; fedha zao zinaonekana kwenye elimu na afya. Hata hivyo, leo wananchi wanalipa kodi, lakini wakienda kwenye afya, dawa hakuna; vifaa fulani, hata Muhimbili, hakuna! Hospitali kubwa ya Rufaa kama Muhimbili unaambiwa vifaa fulani hakuna! Wananchi wanalipa kodi! Inawaumiza ndani

ya nyoyo zao wananchi! Halikubaliki! Unaambiwa kila kitu hapana, hapa hapana! Wananchi wanatoka Mikoani, wanakuja hapa Dar es Salaam wakifika dawa hakuna! Sasa kodi zao wanazokusanya zinawanufaisha kiasi gani? Hili ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nikasema kwa vyovyote iwavyo ni lazima mbadilike, lakini sifikiri tena kama mtabadilika wakati huu! Leo Juni, tarehe ya leo, aah, hapa tena tusebirini wakati *inshallah* ufike.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naona ni fedha za maendeleo ambavyo hazipeleki. Hili limekuwa donda ndugu. Nafikiri ni 40%! Sasa hili nalo ni tatizo. Ni kwa nini mambo haya mnaacha mpaka yafike wakati huu? Tunakoelekea Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mimi namwelekea Spika, nawe uangalie tu nia yangu kwamba kinachokuja hapa, ikiwa fedha za maendeleo ni 40% ni tatizo! Ina maana sisi tunachopanga chote hakuna kinachokwenda! Hapa ni kudanganyana tu basi! Ni kudanganyana tu! Serikali ina tatizo! Ndio nasema kwamba, kwa kweli, umefika wakati Serikali imechoka kweli! Mkubali ukweli! Wala siyo maneno ya kuumiza ukasema labda ni matusi, maneno ya kejeli, hamna! Ndiyo uhalisia ulivyo!

Mheshimiwa Spika, mafao ya Wastaafu; pensheni! Mheshimiwa Hamad hapa, Mbunge wa Magogoni nilikuwa namsikiliza kwa makini juzi; Sh. 50,000/= mpaka Sh. 85,000/=, haitoshi, ni ndogo. Angalau mngesema Sh. 100,000/= sawasawa.

Kwa mujibu wa Mdhifiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amesema hapa kwenye Mafao ya Wastaafu ni kwamba, mnapokokotoa mnawapunja, mnawadhulumu. Tangu mwaka 2006, 2007, 2008, 2009, miaka yote; kila ukiangalia *CAG Report*, mnawapunja Wastaafu mafao yao. Kila tukiwaambia, kwa nini mnawapunja Wastaafu? Kwa nini mnawadhulumu? Wizi mtupu! Mnafanya makusudi kumbe, kwani hamna Wataalamu nyie? Wataalamu si mnao! Kumbe mnawaibia makusudi nyie! Kwa nini msiwaongezee? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni mara chache unasikia hapa daftari limeongezeka, limeongezeka, lakini ukija kuangalia, inasema, majalada ya Wastaafu waliokaguliwa, imeonekana kwamba kati ya majalada haya, majalada haya wamepunjwa. Hamwoni aibu, hamwoni haya nyie! Wazee maskini wa Mungu mwawatia umaskini na ufukara na watoto wao! Hiyo siyo aibu ya mchana kweupe! Tatizo nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wajirekebishe hawa! Lakini sifikirii tena, wakati waliofikia, jua la Alasiri, Magharibi tena na uchaguzi keshokutwa, sifikirii! Saa hizi wako katika mchakato wa mafao ya wazee. Mafao ya wazee hasa, Serikali

inasema iko katika mchakato wa kuwatambua wazee! Tangu mwaka 2010 hapa nikiwa Mbunge mie, Serikali ilisema kwamba wako katika mchakato wa kuwatambua wazee! Mpaka leo wazee hamjawatambua tu! Miaka mitano! Wazee wangapi Tanzania nzima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara hii kwa sababu uchaguzi umeshaanza kukaribia sasa, wanasema wanawatambua! Wanatafuta kura tu za wazee hawa! Hawana chochote walichonacho! Wazee kuwatambua kwani wote ni wangapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mzee akiwa na macho mekundu katika Kanda nyingine huko wanapata matatizo ya kushambuliwa na watu, ndiyo mnatambua sasa ni wazee kwa sababu tayari wameuawa. Watambueni wazee kwa maslahi yao! Leo mchakato wa muda wa miaka mitano hamjawatambua. Mwandae sera, mwandae sheria, itakuwa mpaka lini? Sasa hili nalo ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo kuna mambo ya viwanda vya korosho vya Lindi na Mtwara; mlikopa dola bilioni 20, kutoka Italy na Japan! Viwanda vile mmeviuza! Je, bei ambayo mlikopa na bei mliyozia viwanda vile mmelipa kule? Mliweza kulipa au mligawana wenyewe kwa wenyewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila siku tuna Viwanda vya Lindi na Mtwara vya Korosho! Mlikopa dola bilioni 20, hadi leo mmekwenda mkagawiana, mwajuana ninyi wenyewe. Juzi nikasema kuna viongozi, Mheshimiwa Kafulila akasema aah, usiseme kama ni vigogo! Sasa kwa nini mnapeana? Deni mmeshalipa viwanda vile? Bei ambayo mlikopa: Je, mlipouza mliweza kulipa? Hakuna. Hilo ni tatizo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la ushuru wa Wazanzibari wanaoleta bidhaa za bandari Dar es Salaam. Kuna taarifa wananchi wamesafirisha bidhaa ikiwemo mashine za boti zile, walipitisha pale, lakini bidhaa ilikuwa zisitozwe kodi, lakini sasa unaambiwa kwamba kuna tatizo hili! Sasa hili tatizo nalo ni tatizo kubwa. Mlikubaliana bidhaa za uvuvi hizi na hata Waziri amesema mara nyingi tu hapa, lakini hakuna kilichopo!

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nataka niseme tu kwamba sisi tuna haki ya kushinda dola na masanduku ya kura mwaka huu hayaibiki, tuwaambie kabisa. Masanduku ya kura hayaibiki, tuwaambie kabisa. Tunakwenda katika uchaguzi wa kistaarabu hatuna pingamizi.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda katika uchaguzi; tunataka uchaguzi wa haki na sheria. Tutaendelea kulinda amani na usalama, lakini suala la masanduku ya kura kuchukuliwa kwa wizi, hilo hatukubali. Wala msifikirie kama

tunang'ang'ania Ikulu; wananchi wenyewe ndio watakaotupeleka Ikulu. Wameona upungufu wenu kwa muda wote! Wameona udhaifu mkubwa! Maendeleo mnayoyasema ninyi ni jambo la kawaida! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hili niwaambie tu kwamba tunaelekea katika Uchaguzi Mkuu, lakini katika yote, tisa! Tukubaliane kwenda katika uchaguzi wa kistaarabu. Tusioneshane ubabe kwa sababu ya dola; twende katika uchaguzi wa kistaarabu tukubaliane twende vizuri. Sisi hatuna pingamizi kama UKAWA. Sisi tukishindwa kihalali, tutakubali kwamba tumeshindwa, lakini mkitufanyia varange, mkatufanyia wizi wa makusudi na hilo na sisi ni binadamu, tumeshachoka! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, niseme tu kwamba kwa hali halisi ilivyo, sisi mwaka 2015 wananchi wanatusikiliza, watuunge mkono Vyama vyetu hivi vya UKAWA, ndio tegemeo pekee na ndiyo tumaini letu. *Inshallah Bismillah* na utukufu Mwezi huu wa Ramadhani, naona tutafikia lengo lililokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

SPIKA: Haya. Sasa namwita Mheshimiwa Esther Matiko, halafu tutaona itakavyokuwa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijalia uhai na leo kusimama na kuchangia bajeti kuu ya Serikali kwa maana ndiyo itakuwa mara yangu ya mwisho kwa maana ya kuchangia bajeti hii.

Pia, nachukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Tanzania kwa imani kubwa waliyotupa sisi CHADEMA kuanzia 2010 mpaka sasa hivi, lakini zaidi baada ya mchakato wa Katiba, imani kubwa ambayo wanatupa sisi UKAWA. Nawashukuru sana, nawaambia waendeleo hivyo hivyo na wajitokeze kwa wingi kwenye kujiandikisha katika Daftari la BVR ili tuweze kwenda kuindoa Serikali ya Chama cha Mapinduzi madarakani.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo kuhusu BVR. Tunatambua kwamba mchakato wa BVR unaendelea kwa maana ya kuwaandikisha Watanzania nchi nzima, lakini kumekuwepo na mambo ambayo siyo mazuri. Kwa mfano, kumekuwepo na kusuasua sana kwa uandikishaji; Watanzania wanaamka saa 9.00 wanakaa mpaka saa 12.00 jioni hawajaandikishwa. Hata hivyo, zaidi kumekuwepo na kutakikana kwa Maaskari waliojiandikisha wanaombwa namba zao za vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, tulitaka kujua ni kwa nini mnawaomba Maaskari hawa namba zao za vitambulisho walivyojiandikishia? Kwamba, mnawa-*threaten* wasiende kupiga kura au mnataka kuja kuchunguza wameipigia UKAWA au nani? Tunapenda kujua ni kwa nini Maaskari hawa wanaombwa namba za uandikishwaji?

Mheshimiwa Spika, lingine, kumetokea mkanganyiko, mathalan Tarime kwenye Kata ya Kenyamanyori, wananchi wa Mtaa wa Ronga walienda kuandikishwa Mtaa wa Chira na wanaandikishwa kama wanaishi kwenye Mtaa wa Ronga. Tunapenda kujua, ni kwa nini mnafanya hivi? Kwa nini wasiandikishwe kwenye mtaa husika? Au kama hata kituo kimewekwa huko, ni kwa nini basi wasiweze kutambulika kwamba wanatoika kwenye mtaa wa Ronga na siyo kuandikishwa kama wanatoka kwenye Mtaa wa Chira? Haya yote naona kwamba ni mianya mnatafuta ili mweze kupenya. Lakini mwaka huu hamwezi kupenya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nichangie kwenye hii bajeti ya Serikali. Naenda kuchangia na nikizingatia kama tumekuwa tukiwashauri sana Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, tukiwapa vyanzo mbadala vya mapato kwa miaka mingi tangu Serikali hii ya Awamu ya Nne, lakini inaonekana hawataki kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mianya mingi sana ya mapato. Mathalan utaweza kuona kwamba *wealthness* ya Mtanzania, kwa maana ya utajiri wa Mtanzania alionao ukienda ku-access analipaje kodi yake, utakuta kuna wengine hawana kabisa historia ya kulipa kodi, zaidi labda amelipa kodi wakati anaingiza gari.

Hili tumelisema kwamba, angalao mweze kubuni kwamba mnamiliki; kwa mfano, mathalan Esther Matiko, nina jumba la Shilingi bilioni mbili, nimelipa kodi kiasi gani? Hamfanyi hicho kitu! Hii inapelekea kuwepo fedha haramu.

Mheshimiwa Spika, mngekuwa mnafuatilia kuhakikisha *wealthness* ya Mtanzania *i-reflect* ulipaji kodi wake, leo hii msingeweza kwenda kupandisha madizeli, petroli na mfuta ya taa kwamba eti ndio mweze kufanikisha zoezi la REA.

Mheshimiwa Spika, lingine, tunatambua kwamba kuna Watanzania ambao wamewekeza kwenye majengo, wanapangisha. Kuna wengine wamewekeza kwenye vibanda; maduka. Unakuta mtu anapangisha duka, kijibanda kwa mwaka Shilingi milioni 18, lakini halipi hata *single cent* kwa maana ya kwenda TRA. Hizi zote mngeweza kuzifuatilia vizuri, kuna wengine wandalipwa hata zaidi ya Shilingi bilioni 200, lakini hawalipi kodi! Kwa nini msiende kuzifuatilia hizo mweze kupunguza hizi kodi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mkifuatilia vizuri huko, mtapata fadha nyingi sana kuliko za mafuta ya dizeli, petroli au mafuta ya taa. Tumekuwa tukishauri na mengine mengi mfuatilie mwone; *property tax*, mfuatilie mwasaidie Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeendelea kuona sehemu ambayo ni vyema kupata kodi ni kwa wafanyakazi wanyoge ambao ndiyo mna uhakika wa kukusanya kodi zao kupitia *Pay As You Earn*. Tumeshauri sana muwashushie hawa watu ije kwenye *single digit*, angalao mfikie 9%, lakini mpaka sasa hivi mpo 11%, hatuikubali! Mwendeele kuwashushia ili iweze ku-*reflect* angalau na wale mlivyowashushia kwamba chini ya Shilingi milioni nne wasilipe chochote na wafanyakazi nao mwazingatie kwa sababu, wao pia kwanza hawakwepi kodi! Maana lazima ikifika mwisho wa mwezi lazima watalipa hiyo kodi.

Mheshimiwa Spika, kingine ukiangalia wafanyabiashara wakubwa na wa kati kwenye maduka mengi ukipita hawalipi kodi. Hawakupi hata risiti inayoonesha kwamba wanalipa kodi yoyote ile. Kwa hiyo, unakuta uzembe mkubwa unatokea. Leo, hata ukifanya *research* Dodoma, uende ununue kwenye ma-*super market* na sehemu zote, hupewi risiti ambayo inaonesha kwamba unalipa kodi! Sasa tunaiomba Serikali kabisa, mhakikishe kwamba Watanzania wanalipa kodi.

Mheshimiwa Spika, hata jana watu waliongea hapa kwamba hawa wafanyabishara wanatumika kama tu *agency*. Waelimisheni waweze kulipa hizo kodi na Watanzania pia waweze kuelimika ili mwepukane na kuwapunja Watanzania maskini kwa kuwawekea tozo za mafuta ya taa, tozo za dizeli na petroli. Kwa hili naomba kabisa tuondoe hizi tozo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwenye petroli, Mheshimiwa Waziri unasema kwamba, unaweka kwa vigezo viwili; kwanza uchakachujaji, lakini pili unaongeza ili ziende REA! Ukizingatia REA kwanza, nilisema hata kwenye hotuba yangu hapa, hampeleki hizo fedha. Kwa sababu hampeleki fedha REA, fuatilieni hiyo mianya ambayo ni ya ulipaji kodi huko kwingineko mwondoe tozo, siyo tu kwenye mafuta ya taa, hata kwenye petroli na dizeli, muwarahisishie Watanzania wa kawaida. Kama mkiona sivyo, mfanye kama mlivyofanya kwenye Maabara!

Mheshimiwa Spika, ni bora hata mwainishe ni kiasi gani watachangia Watanzania kupata umeme. Maana mmeenda mmeweka nguzo kule, hata hamjasimamisha, hamna umeme. Bora mwaombe wachangie kwa hiyari wajipatie umeme, kuliko kuwaka kwenye mafuta ya dizeli, ya petroli na mafuta ya taa ambapo mnaenda kuwaumiza Watanzania kwa kiasi kikubwa na mwisho wa siku hiyo REA yenyewe haitafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee pia kwa kuzungumzia sasa mradi wa kimkakati. Nikikaa huku ndani nikaona Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanaitetea Serikali, najiuliza mara mbili mbili; hivi tunajua jukumu letu kwamba tunatakiwa tuisimamie Serikali bila kujali sisi ni wa CCM, sisi ni wa CHADEMA, sisi ni wa CUF au ni wa akina nani! Mtu anasimama anajivika koti la Serikali!

Mheshimiwa Spika, wameainisha kwamba katika mradi wa kimkakati, eti reli; kwa miaka mitano ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa bado wanaendelea kusema wanatenga fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu na kwa ajili ya usanifu wa kina. Ni dhahiri Kambi ya Upinzani Bungeni inasema siku zote kwamba ili tuwe na uchumi imara lazima tuboreshe miundombinu ya usafirishaji kwa maana ya bandari na reli. Lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaonekana kabisa imevaa miwani ya mbao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo wanatuambia baada ya miaka mitano utekelezaji wa mpango wa Taifa, watatenga zaidi ya Shilingi bilioni 28.8 kwa ajili ya upembuzi yakinifu, kwa ajili ya usanifu wa kina, ili kuweza kuboresha reli! Ndani ya miaka mitano unatenga fedha kwa ajili ya mishahara na posho. Unajua kabisa kama ungekuwa unathamini mchango wa reli kwenye uchumi wetu, leo ungetakiwa uwe umeshaboresha reli zote.

Mheshimiwa Spika, kwa mtindo huu, kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, maana kama mwaka 2011/2015 upembuzi yakinifu, ina maana 2015/2020 kama wananchi wa Tanzania wataipa CCM, ina maana watakuwa wanatafuta washauri waelekezi, 2020/2025 wanatafuta Wazabuni. Kwa maana hiyo nchi yetu haitasonga. Ndiyo maana tunasimama hapa tunasema ni wakati sasa Oktoba, 2015 tuwaondoe CCM tuweke watu walio tayari kutumia rasilimali za nchi yao kuwaneemesha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo reli ungeiboresha ungeweza kukwepa uharibifu wa barabara na ajali mbaya zinazotokea. Hata juzi kule kwako Mheshimiwa Spika, wananchi zaidi ya ishirini na kitu wamefariki, chanzo pia ni kukwepana na Lory. Tuki-assess ajali zote zinazotokea Tanzania, nyingi zaidi ya 80% zimetokana na sababu ya kukwepa Lory. Hata Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Marehemu Regia, alifariki kwa kukwepana na malori. Yale malori yangesitishwa, tungekuwa na njia ya reli tungepunguza siyo tu kwamba uharibifu wa barabara, lakini Watanzania ambao ni nguvu kazi ya Taifa, tusingewapoteza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sababu ya Chama cha Mapinduzi, maisha ya Mtanzania kwao ni kitu ambacho hakimati *(matter)* sana. Ukiangalia miundombinu yote ya elimu na afya, ambapo watu wanafariki, hawaboreshi!

Mheshimiwa Spika, niendeleo kwenye BRN. Chama cha Mapinduzi wanasema, mafanikio makubwa, BRN, wanajinasibu! Huwa saa nyingine nikikaa nasema, hivi wanajua kwamba Watanzania hawaelewi au wanafanya makusudi? Tunakuja humu ndani, tunatenga Bajeti, wanatuambia kabisa kwenye mipango yao, kwa mfano, kwenye maji tunatenga Bajeti, lakini baada ya muda hawapeleki fedha, mpaka mwaka unakaribia kwisha. Sasa hivi wamenichekesha zaidi, hata kabla hatujamaliza hili, tumepitisha bajeti hapa, tena tukilalamika kwamba, fedha hazitoshi! Hatujaondoka kwenye Bunge hili, wameshaleta *addendum*.

Mheshimiwa Spika, kwa hili niseme, juzi nilivyokuwa nyumbani nilikuwa naumwa nikamwona Mbunge wa CCM, Mheshimiwa Mangungu, anasema: “mnasema tumeleta *addendum* wakati na nyie mmeleta *addendum*!” Nikasema huyu mtu anajinasifu hivi, hivi anaelewa anachozungumza? Sisi tukileta *addendum* Upinzani, hatujaleta huku mkapitisha. *It is a proposal we are giving to you!*

Mheshimiwa Spika, kama tumekosea, tunaleta tuwaelekeze, lakini hizi zenu mnazoleta, mmetupotezea muda, tumepitisha Bajeti huku tunarudia mara mbili mbili, haijapita siku, mnaleta mnabadilisha kwenye fedha za maendeleo. Mbaya zaidi, bora hata mngebadilisha kwenye fedha za matumizi ya kawaida, mnabadilisha kwenye fedha za maendeleo! Maana yake ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye BRN hiyo hiyo, niongelee kuhusu elimu. Leo miundombinu ya elimu ni mibovu sana na ninafikiri mna ma-TV huko kwenu, mnaona hata HakiElimu wana Tangazo moja la chool!

Mheshimiwa Spika, kile choo kama kweli nyie Mawaziri mna huruma na mna utu na kile choo wanachotoa HakiElimu ni afadhali kuliko vyoo vingine vya Shule za Msingi huko vijijini. Mwalimu anashindwa hata kukanyaga. Wanafunzi wanakanyaga kile choo kina kinyesi, mikojo na kila kitu; wengine wanajisaidia nje ya choo! Halafu mnakuja mnasema BRN imefanikiwa kwenye elimu! *Are you serious guys!* Hatuko *serious* na nchi yetu, kabisa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanasema BRN imefanikiwa kwenye kilimo. Kwenye kilimo chenyewe wanatuambia wamepima mashamba mawili ya Bagamoyo sijui na Mkulazi, eti wamefanikiwa kwenye BRN! Kwenye BRN eti kilimo cha mpunga kutoka tani nne mpaka tani nne na nusu, BRN imefanikiwa.

Jamani! Hivi kweli tumelaaniwa; tumeamua ku-*cease mind* zetu; hatuwatumii Wataalamu wetu; au ni nini? Labda tuje tuweke maombi ya nguvu kabisa kwa sababu tunaelekea kwenye uchaguzi. Mungu atufumbue, tufumbuke, tuweze kuwa tuna-*document* vitu ambavyo tunajua ni kweli vinaenda kuisaidia Tanzania.

Mheshimiwa Spika, leo Mheshimiwa Rais amekwenda London *Summit* akasema kabisa kuhusu uzazi wa mpango kwamba ataweza ku-boost mpaka asilimia 60 na mkasema mtatenga bilioni 20 kila mwaka, lakini kipindi ambacho tumepitisha bajeti kubwa ilikuwa ni bilioni 4.6 na ambazo hamkuzitoa na mnajua kabisa kama mngeweza kutoa zile fedha na mje mtuambie hapa kama mngeweza kutoa fedha za uzazi wa mpango angalau, mka-*invest heavily* na mkawaelimisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mathalani leo Watanzania mia wanapata ujauzito ambapo miundombinu mnajua ni mibovu hamja-*invest* kwenye miundombinu kuliko hawa Watanzania mia wanaopata ujauzito leo na wanafariki kumi, mngeweza kuwashauri labda kwa mwaka wakapata ujauzito Watanzania 30, tungeweza ku-*save* hivyo vifo vya nanihi. Sasa hata kama bilioni 20 mnashindwa ku-*invest* mnategemea nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pensheni, pensheni wanakuja hapa wanasema wameongeza 85, asilimia 70 huyu baba anakaa kijiji ambapo atatumia sh. 10,000 kuja benki, maana yake mabenki hayako vijijini. Akifika benki atumie tena sh. 10,000 kurudi Sh. 20,000 tayari hajala na saa nyingine akija mjini anaweza akalala, anarudi na kale sh. 50,000. Hiyo sh. 50,000 yenyewe dola ipo juu, anakwenda kuishi vipi? Kwa hiyo, tunaomba muwasaidie hawa wazee pandisheni mpaka sh. 150,000 hata siyo sh. 100,000. Pia tuwa-*consider* na wale wazee ambao walikuwa hawafanyi kazi, tunaanza na wenyewe kuwasaidia vipi?

Mheshimiwa Spika, nimalizie katika barabara ya mradi wa *DART*, mradi ule ya Dar es Salaam, nashangaa huwa tunasafiri hata mje mwende hata Kenya tu hapo, jamani ile barabara ilivyojengwa, kwanza ukianza Kimara sijui ile mitaa mingine kati ya Kimara pale hawajaweka upenyezo wa watu wanaotembea kwa miguu, wala pikipiki wala baiskeli. Unavyozidi kuja kwa huku unakuta ile barabara inazidi kupungua, yaani ukipishana na malori mawili ambayo ndiyo mnaendelea kuyabeba kwasababu sijui mmewekeza huko kwenye malori, hayawezi yakatembea ma-*semi trailer* mawili yakafika, kona zake zile ziko *sharp* sana. Mtu akifika pale na gari akapata *tyre bust* lazima anadumbukia kwenye shimo na ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho wa siku, naongea hili na najua Mwenyezi Mungu atanisimamia nitarudi Bungeni, ile barabara ina ufisadi wa kufa mtu, tutakuja tutaongea Bunge lijalo hapa na naomba kabisa uchunguzi wa kina ufanyike, huu mradi wa *DART* watu wamepiga mabilioni, yaani hiki ni ki-*ESCROW* kidogo, ni ki-*EPA* kidogo, ndiyo maana nasema hatuko *serious* na mambo yetu kama vile ambavyo wamepiga fedha kwenye bomba la gesi....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Haya ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Alhaji.... Mheshimiwa Mangungu. Mheshimiwa Dkt. samahani kidogo tu.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nilipenda tu kumtaarifu msemaji aliyepita ambaye alikuwa amenitaja kwa jina hasa, kwamba *addendum* ambayo ilikuwa inazungumziwa Serikali ilileta wao walikuwa wakiishutumu Serikali kwa nini wameleta kiraka hali ya kuwa na wao wameleta. Hawa ndiyo ambao niliwatamka wana njaa ya kufikiri.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, endelea na mjadala!

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia machache katika Wizara hii. Kwanza kabisa kabla sijaendelea, napenda niwashukuru wananchi wangu wa Wilaya ya Katavi kwa imani kubwa wanayoionyesha juu yangu na najua watanirudisha kupitia Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, napenda nikupongeze wewe mwenyewe kwa upendo wako na kwa namna ya pekee ambavyo umekuwa ukinielekeza shughuli za hapa Bungeni na hadi sasa naweza kusema nimekoma kisiasa na nakupenda sana mama yangu. Nakuomba uendelee na kazi na Mwenyezi Mungu akujalie maisha mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, napenda sasa nianze kuchangia mpango huu kwa kuanza kabisa nasehemu ile ya kwanza ya dhamira ya Serikali ya kuongeza makusanyo ya mapato. Katika sehemu hii Serikali imesema itaweka mikataba, utendaji na TRA ili kuhakikisha inafikia malengo. Mikataba hii ipo na tumekuwa tukiona malengo haya namna ambavyo yanafikiwa. Wakati mwingine inafika mahali tunasema sekta fulani au TRA wamekusanya kwa asilimia 90 au kwa asilimia 100. Je, ni kipimo gani kinaweza kutuonesha kwamba hayo ndiyo yalikuwa malengo? Inawezekana walikusanya wakafika 150, lakini nani anayefanya udhibiti? Kwa hiyo, naomba katika hili Serikali iangalie utaratibu vizuri wa namna ya kuweka mifumo hiyo ili kuhakikisha kweli tunapata makusanyo ya mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, lingine napenda niende moja kwa moja kwenye tozo kwa ajili ya majengo. Niiombe Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Wizara hii ya Fedha, iangalie upya ni namna gani sasa mtaweza kuangalia viwango stahiki kwa namna ambavyo watu watakuwa wameendeleza maeneo yao katika

masuala ya majengo kwa ujumla. Kwa mfano, tumekuwa na tozo nyingi sana, tozo za viwanja, tozo za nini zimekuwa zikipanda mara mbili, mara tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unapofika kumwambia mwananchi wa kawaida kwamba sasa umelipia kiwanja, lakini unatakiwa ulipie na nyumba aliyojenga mwenyewe, kidogo inatusumbua katika kukusanya mapato. Kwa hiyo, niombe kabisa kama kweli tuna nia ya kukusanya mapato katika hivi vyanzo, tuangalie utaratibu mzuri ambao kila mtu atalipia kwa staili kutokana na alichowekeza katika ile ardhi.

Mheshimiwa Spika, pia niishukuru Serikali kwa namna ambavyo imekuwa ikisikiliza kilio cha Waheshimiwa Wabunge wote ambao tumekuwa mara nyingi tukisema kwenye suala zima la maslahi ya wananchi, kwamba ipunguze kodi kwa kima kwa chini kutokana na kwamba tumesema wafanyakazi ndiyo moja kwa moja ambao wanalipa hizi kodi kwa sababu wenyewe hawana ujanja mwisho wa mwezi lazima kodi ile ikatwe.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naishukuru Serikali imekuwa sikivu na imeweza kufuatilia, *of course* hatuwezi kupunguza kwa mara vupu, hapana, tunakwenda kwa utaratibu na nashukuru kwa utaratibu ambao imeazimia. Kwa mfano, kutoka asilimia 12 kwa mwaka uliopita mpaka asilimia 11, naamini namna tunavyokwenda tunaweza tukafika hata asilimia saba ama asilimia tano. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa hatua hiyo ambayo inaweza kwenda.

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja pia niangalie katika kima cha chini cha wastaafu, Serikali imejitahidi. Kama nilivyosema, hatuwezi kuongeza kwa mara moja, lazima twende kwa utaratibu ambao tunafikiri utatufikisha mahali ambapo tutafikia kiwango kizuri kwa ajili ya kuwawezesha wananchi wetu. Kwa hiyo, pia niipongeza Serikali kutoka sh. 50,000 mpaka sh. 85,000 si haba ni hatua nzuri, ni hatua za mwanzo.

Mheshimiwa Spika, vile vile niangalie utaratibu ambao Serikali imeweka kwa ajili ya mafao ya wazee, napenda tu niombe Serikali sasa kwa kuwa sasa inakuja na utaratibu mzuri wa kuangalia hawa wazee wanapata mafao yao kiasi gani, niombe ombi moja, kuanzia kwenye wastaafu mpaka kwenye haya mafao ya wazee, Serikali iharakishe mchakato huu ili iwatambue wazee hawa haraka mapema na waweze kupata mafao yao. Pia iainishe ni wazee wa aina gani wanatakiwa kupata kwa sababu imekuwa ikitusumbua, kwa mfano, huu mpango wa *TASAF* awamu ya tatu, umekuwa ukitusumbua sana kwa upande wa wazee. Kuna hii suala la matibabu ya bure, kwa wazee napo wakati mwingine wanakuwa hawaelewi, wanafikiri ndiyo pensheni zenyewe. Sasa naomba muangalie namna ambavyo mtaweza.

Mheshimiwa Spika, kwenye masuala ya matumizi ya hizi mashine za *EFDs*, kidogo imeonesha kuna tatizo, lakini niombe Serikali sasa iongeze kasi ya kutoa elimu, jamani nchi hii lazima ijengwe kwa kodi! Hatuwezi mtu mfanyabiashara anasimama tu anasema mimi silipi sh. 40,000 nitalipa sh. 5,000 haiwezekani, tufike mahali tukubaliane lazima tulipe kodi ili tupate maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kabisa haya matumizi ya hizi *EFDs* yafanyiwe utaratibu na wananchi wapate elimu. Naamini Watanzania ni waelewa na ukiwaelimisha, ukiwaelekeza watakusikiliza, tusitumie nguvu katika kuwaelimisha, tutumie busara na tuwape umuhimu wa kodi na nafikiri wanaelewa ni ujanja ujanja tu wa kutengeneza *super profit*. Kwa hiyo, niombe kabisa Serikali ilianganalie hilo na hatuna sababu ya ku-*give up* kwa sababu tunahitaji kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba niliongelee hili suala la kupanda kwa tozo za mafuta. Tufike mahali tuanganalie, nataka tu kuuliza humu ndani, ni Wabunge wangapi humu ndani wana majiko ya Mchina wanaotumia mafuta ya taa. Turudi vijijini ni wanavijiji wangapi wanaotumia majiko ya mchina kwa mafuta ya taa, tukiangalia sana utakuta ni kuni na mkaa. Tufike mahali twende kwenye *reality* kwenye ukweli, mimi ukiniambia kwamba hizi pesa haziendi *REA* nitashangaa, *REA* imepata kutoka asilimia saba mwaka 2011 hadi asilimia 36 mwaka 2014, wananchi wana umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tufike mahali kizazi hiki tulichoko sasa tuingie hizi gharama kunufaisha kizazi kijacho, tufike mahali tukubali hizi gharama sasa. Maana yake lazima tufike mahali sasa kuna kizazi lazima ki-*sacrifice* kwa ajili ya kizazi kijacho, ndiyo tunasema maana ya maendeleo endelevu tufanye haya leo kwa ajili ya *future generation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusifike mahali tunafikia tu, tuumie, tuumie sasa hivi, tufike asilimia 50, mpaka 70 ya wananchi vijijini kupata umeme. Kwa hiyo, tusinanii kwa sababu kwanza tutasema anapikia jiko la mchina ama amewasha koroboi, ule moshi ni *carbonmonoxide*, unamduru kifua, utamduru maradhi mengine ndani ya mwili, sasa tufike mahali tuweke umeme. Naamini hawa watu wa *REA* hawawezi kuwa na makusudi hizi hela zisiende. Kwa hiyo, niombe Serikali, ifike mahali sisi vijijini kule tunahitaji umeme, nguzo zipo ndiyo sasa hii hela iende ikaweke kule umeme tupate umeme. Kwa hiyo, naomba kabisa tuendeleo na hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nije kwenye masuala ya mipango ya maendeleo, tuna dira ya maendeleo, niombe Serikali hatuna sababu ya kuingia humu leo, tunapanga hiki kesho Waheshimiwa tukasema hiki kikabadilishwa, hebu Serikali iwe na mkakati, iwe na mipangilio, kuwe na

consistency kama tumeanza mradi huu basi tuhakikishe tunaumaliza. Kama tuna miradi ya kimkakati ya Kitaifa tuhakikishe tunamaliza.

Mheshimiwa Spika, sasa tuko kwenye reli, sawa naishukuru tumenunua mabehewa, tumenunua vichwa, sijui tumefanya nini lakini turudi kwenye agenda yetu ya msingi ya reli ya kutandika reli ya *standard gauge*. Turudi pale hatuna sababu sasa miaka mitano ijayo tunakatiza hili tunaanza lingine, haya tuliyoyapanga tuendeleo nayo, tuhakikishe tunafikia mwisho.

Mheshimiwa Spika, bila reli, bila bandari kwa kweli tutaziumiza barabara zetu ambazo zimekuwa zikitengenezwa kwa gharama kubwa sana. Kwenye masuala ya madaraja, tuhakikishe yanakwisha, daraja langu la Kavu kule, la Inyonga Majimoto, nimekwisha lipigia kelele mpaka siku hizi wananiita mamaa wa Kavu, mamaa wa Majimoto. Sasa nawaombeni hili daraja liende likamalizike liwasaidie wananchi kule na liko mpango humu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije kwenye maendeleo, mipango ya maendeleo ya rasilimali watu. Napenda kuishukuru Serikali yangu kwani imekuja na mpango kabambe wa kuanzisha maabara mashuleni. Niiombe Serikali, maabara peke yake haiwezi kwenda peke yake kwa ajili ya kudumisha ama kuboresha elimu, niombe sasa katika kufikiria na niwaombe ndugu zangu Watanzania, sasa ndiko kwenye kuwekeza huku kwenye rasilimali ya watu, niwaombe sasa tumejenga vituo vya afya kila Kata havina wataalam. Wataalam watapatikana kwa kuendeleza hizi maabara.

Mheshimiwa Spika, sasa niwaombe tuhakikishe maabara zetu za shule zinakwisha ili watoto wetu tuwawekeze vizuri kwenye elimu, tuhakikishe maabara zile zinakwisha, lakini si tu maabara kwisha, ziende sasa sambamba na maabara za kompyuta na isiwe tu sekondari, turudi kwenye mipango ya shule ya msingi pia nako tuwe na maabara ili mtoto aweze kutofautisha mchicha na ua, aanze kuanzia shule ya msingi. Kwa hiyo, niwaombe iende pia sambamba na nyumba za Walimu ili angalau Mwalimu naye aweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye miradi ya maendeleo ya maji, sijajua ni nini kinatokea ndani ya Mradi wa Vijiji Kumi katika kila Halmashuari, huu mpango unaonekana kama unasua sua. Niiombe Serikali iangalie namna ambavyo itaweza kutekeleza hii miradi, najua ni hela za wafadhili, hela ya mfadhili huwezi kuibadilishia matumizi. Hata hivyo, kuna maeneo mengine inawezekana kuna maji ya mtiririko tunafanyaje, kama tunaweza tukaomba hata vibali tukabadilisha hizi hela matumizi yake kutoka kwa wafadhili itakuwa ni vyema.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwangu kule Mamba mpaka Majimoto, tunaweza kutumia maji ya mtiririko, kwa Mheshimiwa Malocha kule Kilida mpaka Kamsamba kule unaweza kutumia maji ya mtiririko. Kwa hiyo,

niwaombe, kama tunaweza tukawaombea vibali, hizi pesa za vijiji kumi tukazibadilishia matumizi yake kule ambako hatuwezi kuchimba visima tukaweka mradi wa maji ya mtiririko, mtakuwa mmetusaidia sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na narudia kusema tena, nakupenda sana mama yangu. Ahsante. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Alhaji Missanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Khamis Seif!

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, *Bismillah-ar- Rahmana-ar-Rahim*. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataallah*, kwa kunijalia afya, uzima na salama na kuniwezesha kusimama mbele yako ili kutoa mchango wangu katika agenda hii tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, pili, leo ni mwezi pili mwezi wa Ramadhan nami niungane na Waislam wengine wote kuwatakia kila kheri katika mfungo mwema kwa mwezi huu na *Inshallah* Mwenyezi Mungu atujalie yale ambayo tunayakusudia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake wote wawili, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii ya Fedha na taasisi mbalimbali kwa maandalizi mazuri ya bajeti ambayo wametuletea, wamejitahidi kiasi cha kutosha kama ilivyoelezwa na wenzangu kwamba angalau wamethubutu kuondoa lile jina ambalo lilikuwa linaitwa bajeti ya bia, bajeti ya soda na bajeti ya sigara, ama la, angalau wamethubutu. Kwa hiyo, katika rekodi Mheshimiwa Waziri Mkuya, ataingia kwenye rekodi kwamba amethubutu kuondoa neno la bajeti ya bia, bajeti ya soda na bajeti ya vinywaji vingine na *sharab* zingine zingine zile, hongera sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kazi iliyopo ni kusimamia yale ambayo tumeyapanga. Tupo kwenye mchakato wa uchaguzi, nina wasiwasi kwamba *focus* mawazo ya viongozi wakuu wa Serikali na taasisi mbalimbali wote wako kwenye uchaguzi. Sasa sina hakika usimamizi wa mapato yale ambayo tumeyalenga kwenye bajeti hii yatapatikana kiasi gani. Ningeomba wale watakaokuwepo ofisini Makatibu Wakuu na wengine, wajitahidi vinginevyo haya ambayo mazuri tumepangiwa hapa hayawezi yakapatikana.

Mheshimiwa Spika, uko wasiwasi wa wahisani wetu, wafadhili wetu, kusita kutoa fedha zile za mikopo na zingine za uhisani kwa sababu ya wasiwasi wa uchaguzi. Kwa hiyo, kuna vipengele kama viwili, vitatu hivi ambavyo tusipoviangalia vinaweza vikasababisha tukapata upungufu kidogo katika mapato yetu. Kwa hiyo, naomba wale ambao watakuwepo ofisini hasa

Makatibu Wakuu na wengine, kwa kweli wajitahidi kusimamia kikamilifu ili tuone kwamba mapato yetu tunayapata.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Pinda, kwa kukubali maombi yangu. Nilimpelekea maombi yangu na mwenzangu ya ujenzi wa daraja la Minyughe, daraja ambalo limesumbua sana Halmashauri yangu haina uwezo wa kulijenga. Baada ya kuwasilisha maombi yangu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameyakubali, ameyafanyia kazi na tayari amesha-*realize funds*. Kwa kweli namshukuru sana, kwa muda mfupi tayari Mheshimiwa Waziri ametoa maelekezo, tumepokea shilingi milioni 776 kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo kati ya sh. 1,800,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, matumaini yangu ni kwamba, ataendeleza kasi hiyo ili kusudi hizi ambazo zimebakia nazo ziweze kupatikana mapema iwezekanavyo. *Consultant* ameshapatikana kwa ajili ya *designer construction*, atamaliza wakati wowote kuanzia sasa, zikipatikana hizi fedha bilioni moja zilizobakia, nina hakika ujenzi wa daraja hili la Minyughe utafanyika mapema. Kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini nimwombe awakumbushe wale wanaohusika ili watume na hizi fedha zingine.

Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu kupongeza Serikali kwa kuongeza pensheni kutoka sh. 50,000 mpaka sh. 85,000. Ni kweli sh. 85,000 siyo nyingi, lakini ni kweli pia kumekuwa na ziada ya kutoka sh. 50,000 mpaka sh. 85,000.

Mheshimiwa Spika, siku za nyuma niliwahi kushauri kwamba, wenzetu katika nchi nyingine huko suala la pensheni limekuwa *packed* na kima cha chini cha mshahara. Kwamba kima cha chini cha mshahara ndiyo kina-*determine* pensheni ya wananchi, sasa inawezekana kwa uchumi wetu sisi pengine ni mapema sana kuangalia kwamba kima cha chini ya mshahara ndiyo hicho kima chini cha pensheni, lakini angalau basi useme nusu ya kima cha chini cha Serikali ndiyo iwe pensheni. Kwa hiyo, wala hiyo hatutasumbuani hapa kila siku, ongeza pensheni, ongeza pensheni, itakuwa inajulikana tu kwamba kima cha chini cha mshahara kikiongezeka na pensheni nayo inaongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni ushauri wangu, kwanza tupokee sh. 85,000 na tushukuru kwamba Serikali imeonesha jitihada, si haba, lakini huko tuendako, ni vizuri tukaangalia sasa kui-pack hii pensheni na kima cha chini cha mshahara, lakini kwa kuanzia angalau nusu ya kima cha chini cha mshahara, iwe imeeleweka na itakuwa haina matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, vile vile, ombi langu ni kwamba, pamoja na kunyanyua hiki kima cha chini kutoka sh. 50,000 mpaka sh. 85,000, kuna wale waliokuwa katika hapa, matumaini yangu kwamba Serikali nayo iki-*adjust*

pensheni zao *accordingly*. Kwa mfano, yule mtu ambaye alikuwa anapata sh. 80,000 au sh. 90,000 wakati ule, kabla wakati hiki kima cha sh. 50,000, sasa matumaini yangu ni kwamba, utawala bora katika mambo ya *salary administration*, hawa nao watarekebishiwa pensheni zao, wasiendelee kubaki tu pale zile zile sh. 70,000, au sh. 90,000, wakati wenzao wamepanda kutoka sh. 50,000 mpaka sh. 85,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiria kwamba hilo nalo liangaliwe angaliwe ili kusudi wale ambao walikuwa wanapata zaidi ya sh. 50,000, pensheni zao nao ziwe *adjusted accordingly*, wenyewe watalaam wanajua ili kusudi na wao wajione kwamba na sisi tumenufaika kutokana na ongezeko hili la pensheni ambayo...

Mheshimiwa Spika, *equally the same*, wale ambao wako kwenye Mifuko, niombe Serikali, Serikali ndiyo hiyo hiyo, iangalie pamoja na mamlaka inayohusika ile, kuona na zile nazo kwenye pensheni ya Mifuko. Akina PPF, NSSF na wengineo, nao waangalie uwezekano wa kuboresha zile pensheni zao, zisibaki pale *static*, toka mtu amestafu shilingi sijui ngapi, basi ni hizo hizo, ni hizo hizo, hizo nazo zingefanyiwa hivyo, nadhani litakuwa ni jambo la maana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, amesemea Mheshimiwa Waziri, lakini itabidi nirudi kwenye umeme wa upepo wa Singida. Nipo hapa kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa Singida. Sasa ukiuliza, anapiga kelele huyu kwa maslahi ya nani, maslahi ya wananchi wa Singida, hakuna maslahi mengine, kila mtu anapigania maslahi yake hapa. Kwa hiyo, nasema, bado nimwombe Mheshimiwa Waziri, chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli waangalie au wakamilishe taratibu zile za kupata mkopo wa kutoka *Exim Bank*, kwa ajili ya umeme huu wa upepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimetoka Singida, wananchi wanasikitika sana, kwa nini! Mwanzoni, anafahamu Mheshimiwa Waziri hata Naibu Waziri, kulikuwa na *Wind East Africa* ambao walikuwa wamejiandaa kukamilisha umeme huu wa upepo wa Singida. Haijulikani kumetokea nini, urasimu wa Serikalini, mpaka ule utaratibu wa *Wind East Africa* kupata huu mradi wa umeme wa upepo, umetoweka hivi hivi tu, haijulikani kwa nini!

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nasikia wamekuja Wamarekani, kutaka kuwekeza tena katika umeme wa upepo, nao wanapigwa danadana, mara waambiwe sijui omba tena, mara kufanya nini, imekufa hivi hivi. Tukaweka matumaini kwamba angalau huu sasa ambao uko chini ya NDC na TANESCO mashirika, taasisi za umma na wawekezaji wachache tu, angalau sasa wangepanikiwa, baada ya kupita *processes* zote, miaka saba iliyopita, wanakuja kukwamishwa dakika ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, wamekwenda kwenye Tume ya Mipango, kwenye Kamati ya Madeni, sijui kwenye Baraza la Mawaziri, huko kwenye BRN, sasa unajiuliza, hivi processes zote hizi zimefanyika, halafu mradi huu unakufa hivi hivi kienyeji tu basi! Halafu unafikiri sisi watu wa Singida tutakufurahia tu, haiwezekani, hatuwezi kukufurahia, tukufurahie kwa sababu ya nini! Haiwezekani! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nisisitize tena, kwa kweli tuko kwenye kipindi kibaya, wananchi Wanasingida wanajiuliza, hivi tuna tatizo gani, tumepata mradi mzuri, ajira nimesema zaidi ya watu 2,500 kutakuwa na megawatt 300 ambazo zitaingia kwenye grid ya Taifa, ni senti 13, badala ya senti 33 za umeme wa sasa, hivi mnataka mradi gani wenye manufaa kwa nchi zaidi ya huu! Halafu hivi hivi tu from no where mtu anakwenda kuuondoa, au unaondoshwa.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwakilishi yuko pale, kwa kweli nazungumzia kwa chungu, kwamba tafadhali mwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu, asije kule na fomu yake kule, badala ya kumjazia fomu, tukaanza kumpiga maswali ya umeme wa upepo. Atukamilishie hili, akija na fomu zake tunazijaza, lakini swali lazima tumuulize, wapi tumefikia kuhusu umeme wa upepo wa Singida, inaniuma sana, Wind East Africa imekufa, wale Wamarekani wamekuwa frustrated, hawa tena wameondolewa, umeme wa upepo umepeperushwa, umepelekwa sijui wapi huko, mimi hata sitaki kusema. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Posta, ni shirika la umma, toka limeanzishwa mwaka 1993, nilisema last time, hawajapata mtaji hawa! Benki ya akinamama imeanzishwa, imepewa mtaji, sijui Benki ya Posta imeanzishwa imepewa mtaji, tumeanzisha Benki ya Wakulima inapewa mtaji na taasisi nyingi tu zinapewa mtaji. Hawa wana nini, wana tatizo gani hawa?

Mheshimiwa Spika, Sheria inasema, Waziri wa Fedha na Waziri anayehusika na Mawasiliano, watakaa wa-determine mtaji. Toka 1993 to date, hakuna wafanyakazi wanoadhalilika kama wafanyakazi wa posta, I am telling you. Mtu kafanya miaka 30 miaka 40, mpaka leo anapata sh. 300,000, miaka 30, miaka 40, three hundred thousand shillings, basi! Hivi sasa wananufaika na kima cha chini cha Serikali, kipandishwa kile angalau na wao wanaambulia, lakini hawana utaratibu kwa sababu hali yao ni dhofu-l-hali, kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira magumu, vyanzo vya mapato hakuna, hawana msaada wowote, mtaji hawapewi. Tatizo ni nini, kama imeshindikana, jamani, semeni shirika hili sasa tunalibinafsisha asilimia 100, lakini msiwatese wale watumishi ambao wamekwenda kule.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, yeye anayo role, kwa mujibu wa Sheria namba 19 ya mwaka 1993, kuangalia kwamba wana posta wanapata mtaji, kwa kushirikiana na Mheshimiwa Waziri anayehusika.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo niseme, nimefurahi kuona Serikali imesikiliza kilio cha watu kwamba sukari inaingia holela, wamechukua hatua ambazo zitarekebisha suala hilo. Sukari inaingia holela, cement inaingia holela, mafuta ya chakula yanaingia holela, vitu vya anasa vinaingia holela, yaani kama vile hakuna uongozi, hakuna mtawala juu ya hiyo kitu.

Mheshimiwa Spika, sasa hili la sukari nasema pamoja na mambo mengine, nashukuru kwa hilo, lakini tatizo lililopo, tutatunga sheria nyingi sana, tutatunga kanuni nyingi sana, vyombo vilivyopewa kazi ya kudhibiti, havifanyi kazi. Viko vyombo vingi sana ambavyo viko hapa nchini, ambavyo vinatakiwa kusimamia vitu mbalimbali, viko vyombo vingi sana, lakini havifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata Bunge lako Tukufu hili likitunga sheria 200, 300 juu ya jambo fulani, kama vyombo vilivyopewa kazi ya kusimamia masuala yale havifanyi kazi, kwa sababu kwa mfano, tuliambiwa kwenye Kamati yetu ya uchumi, kwamba cement inaingizwa kutoka *Pakistan* na kutoka wapi sijui, hawalipi ushuru na ndiyo maana inauzwa sementi ile sh. 7,000. Vipi utashindanisha na sementi yetu sisi hapa ambayo ina gharama chungu nzima, sasa hiyo ni *unfair competition*. Sasa hicho chombo ambacho kinaitwa sijui Tume ya *Fair Competition*, ipo, lakini haifanyi kazi, cement inaingia bure bila ushuru wowote, TRA wapo, Serikali wapo, ndiyo maana tunapakwa matope tunaambiwa, mradi wa wakubwa huo, hauwezi kusimama mradi wa cement, ndivyo inavyosemwa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuachane na tuhuma zingine ambazo hazina sababu. Kwa hiyo, nasema pamoja na nia nzuri ya ku-control sukari, naomba Serikali iangalie vyombo vile ambavyo vimekabidhiwa kazi ya kudhibiti mambo haya kuingia holelaholela, sukari hizi, cement, mafuta na nini, kwa kweli vinashughulikiwa ili i kuona kwamba bidhaa inayoingia, inaingia kwa mujibu wa taratibu.

Mheshimiwa Spika, riba, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema; hakuna mtu ambaye anaweza kajiendeleza bila kukopa, sasa utamaduni wa kukopa, wengine tunaogopa kwa sababu ya riba. Tumelizungumza miaka nenda miaka rudi, wakubwa wana-defend sana hii riba, interest ni kubwa sana kwenye mabenki. Tunasema tuwape vijana wetu waliotoka shule hawa mikopo ya mabenki wajenge nyumba, wanunue magari, wafanye nini ili waondokane na habari ya kuchukua chao mapema.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kama anakwenda kule anapata *interest* sijui 18, 19, 20, kijana huyo anakuwa *frustrated* hawezi, matokeo yake anatumia kalamu yake sasa ilia pate chake mapema, ajenge nyumba, apate gari, aoe mke mzuri, apate mume mzuri na kadhalika na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, tatizo la riba bado ni kubwa sana na sioni jitihada za Serikali za dhati kweli kweli kabisa katika kuli-address hili suala la riba ili kusudi wananchi wapate mikopo, waweze kufanya haya mambo ambayo wanakusudiwa kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala ujenzi wa ofisi zetu. Singida ni miongoni mwa mkoa ambayo tumepata maeneo mapya ya wilaya, tuna Wilaya ya Ikungi, Wilaya ya Mkalama, kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, atuangalie. Kuna miradi imeshaanza, lakini miradi inasuasua, inaonekana mawasilisho ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya DC, Ofisi za Mkurugenzi, zinasuasua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niombe kwamba, tujitahidi ili tuone kwamba majengo haya yanakamilishwa na yanamalizika.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Ya pili, ya kwanza!

SPIKA: Haya ahsante, ya pili.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru na nakutakia ramadhani njema.

SPIKA: Nami pia. Sasa nilisema nitamwita Mheshimiwa Ali Khamis Seif, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Chombo na Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac-!

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, sina budi kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima na kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu. Pili namwomba Mwenyezi Mungu atujalie uhai na uzima ili tuweze kuifunga ramadhani hii tukufu. Tatu, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, huu ni Mkutano wa Tano, unaohusiana na bajeti katika uhai wa Bunge hili la 20 na tumeshuhudia kila mwaka kwa kweli bajeti inaongezeka. Tumeanza 11 trillioni, tumekwenda 15 trillioni, tumekwenda 18, 19, mwaka huu ambao unaishia Juni, 30, na hii bajeti mpya ni trillioni 22.

Mheshimiwa Spika, sasa katika mtazamo wa ghafla unaweza ukaona kuwa kuna hatua kubwa ya maendeleo inapatikana kutokana na kupanda

kwa wingi wa fedha, bajeti hadi bajeti, lakini ni jambo la kusikitisha kwa kweli, kuwa sijui Wizara ya Fedha ikoje, naamini ina wasomi, ina wataalam, lakini bado bajeti zao kwa kweli wanazotuletea hapa basi haziendani, fedha zinazopatikana kwa kweli hazikubali kabisa na kadri unavyooeleza, basi hakikisha kila mwaka bajeti itakuwa inapandishwa.

Mheshimiwa Spika, nimefanya utafiti mdogo tu kuhusiana na suala hili. Bajeti ya Serikali inajengwa na kwanza na mapato yanayopatikana, lakini katika matumizi inakuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na fedha za maendeleo. Nimejaribu kuona, kwa miaka mitatu, Serikali imeleta nini hapa na hali halisi imekuwaje!

Mheshimiwa Spika, twende katika matumizi ya kawaida, kwa sababu mnapopata matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo hapo ndiyo unapata bajeti halisi ambayo Serikali ilituletea ili tuijadili na hatima yake tuidhinishe katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011/2012, Serikali wenyewe ilieleza kuwa, matumizi ya kawaida yatakuwa ni trillioni 9.21, lakini fedha ambayo imetolewa na Wizara ya Fedha ni trillioni 8.68, hapa kuna upungufu wa bilioni 527.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012/2013, trillioni 8.59 ni fedha ambayo illidhinishwa na Bunge, fedha iliyotolewa na Wizara ya Fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka huo ni trillioni 8.28, ambayo kulikuwa na upungufu wa bilioni 315.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Serikali wenyewe, wakatuletea trillioni 9.59, fedha iliyopatikana ni trillioni 9.55, walikuwa na upungufu wa bilioni 400.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inaonekana Serikali licha ya kuwa na ukosefu wa bilioni 527 bilioni 315 na bilioni 400, lakini bado wanatuletea matumizi yale yale ya kawaida ambayo unakuta yanaongezeka na kishindo, kiko katika matumizi ya maendeleo kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011/2012, Fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge ilikuwa ni trillioni 4.31, zilizotolewa ni trillioni 3.38, kulikuwa na upungufu wa bilioni 926.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012/2013, trillioni 4.72, zilizotolewa ni trillioni 3.27 kulikuwa na upungufu wa bilioni 977.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, trillioni 5.03, zilizotoka ni trillioni 3.14, fedha ambazo hazikupatikana ni trillioni 1.88.

Mheshimiwa Spika, sasa, kama Wizara ya Fedha ingekuwa makini, ni dhahiri inaonyesha kuwa, fedha ambazo au makisio ambayo wanatuletea ya bajeti, kwa kweli yalikuwa hayastahiki, lakini yalikuwa yanafanywa ili ionekane kuwa kila mwaka fedha inaongezeka, bajeti inakua, maendeleo yanapatikana. Hatima yake sasa, katika Bunge hili miradi mingi inazungumzwa, tunafurahi, tunapiga meza, lakini unapokuja katika utekelezaji hapo, fedha haipo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo utakuta kila Mbunge anayesimama anazungumza suala la miradi katika maeneo ya Majimbo, haitapatikana kwa sababu fedha haipo! Leo trillions 1.8 haipo ya maendeleo. Sasa matokeo yake lingine ni kwa Serikali, nina hakika na kama Bunge tutataka kusimamia hili, nina hakika ina miradi mingine imefikia pengine asilimia 25, mingine asilimia 50 na mradi ule baada ya kwa mfano, umalizwe kwa bilioni tatu, basi nakuhakikishia, kwa sababu unachukua miaka mitatu, minne, unaweza ukamalizwa pengine kwa bilioni 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo kubwa, Serikali wameshindwa miaka yote mitano hii kutuletea bajeti, naelewa ni maksio, lakini maksio, yaendane na hali ambayo inaonekana mapato yapo, lakini aaa, tuongeze tu, tuongeze, matokeo yake ndiyo kama haya.

Mheshimiwa Spika, nioneshe mfano, ukiangalia mwaka 2013/2014, jumla ya fedha ambazo, ukichukua matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo, upungufu wake ni trillions 2.28, fedha ambazo hazikupatikana hizo. Bajeti ya mwaka huu, ilikuwa ni trillions 18.24, kwa hiyo, ukitoa 2.28, hapo utapata trillions 15.96, hii ndiyo bajeti hasa ilitakiwa iwe! Yaani upungufu kuna trillions mbili nukta. Kwa hiyo, ni dhahiri inaonesha kuwa, hii bajeti ambayo tunasema ni trillions 22, nasema ni bajeti angalau ingekuwa ya trillions 20, kwa sababu ukisema trillions 22 si kweli. Hii inayoishia Juni, hii, fedha ya maendeleo iliypangwa ni trillions 6.44, mpaka Machi, ni trillions 2.41, hapo ndiyo pana maafa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima Bunge liwe makini katika suala hili. Kamati ya Bajeti ione hilo, kuwa bajeti inayoletwa, haikaribii hata kidogo katika uhalisia wake, kwa hiyo, tunapanga mambo ambayo hayatekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la deni la Taifa, kwa kweli napata mashaka makubwa, licha ya ule ukuaji, lakini tunaambiwa na Serikali hii hii, kuwa tunakopa fedha kwa sababu ya maendeleo, yaani fedha inayokopwa haitumiwi kwa matumizi mengine isipokuwa kwa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nilifuatilia suala hili; mwaka wa 2011/2012 Tanzania ilikuwa inadaiwa trillions 16.50. Ongezeko la deni hili kutoka mwaka 2010/2011 ni trillions 4.33. Fedha ya maendeleo kama nilivyoeleza mwanzo ya mwaka 2011/2012 ni trillions 3.27. Huku ongezeko la deni ni 4.33, lakini fedha iliyopelekwa

kwa maendeleo ni trilioni 3.27, kuna karibu trilioni moja haipo. Kwa hiyo, inaonekana siyo sahihi au siyo kweli wanachotuaambia Serikali kuwa fedha hii inakopwa kwa kuleta maendeleo, kwa sababu mwaka huu ingeonekana kuwa fedha ya mkopo imepelekwa huku tungekuwa na 4.33. Kwa hiyo, hili kwa kweli Serikali hawatuelezi usahihi wake.

Mheshimiwa Spika, napata mashaka zaidi ninapoambiwa Deni la Taifa. Tunaambiwa mpaka Disemba 2014, Deni la Taifa limekua hivi sasa tunadaiwa trilioni 33.6. Halafu utapata mchanganuo hapo kuwa Deni la Serikali ni trilioni 30.1. Deni la Sekta Binafsi, hapa ndiyo penye mashaka ni trilioni 3.5.

Mheshimiwa Spika, sasa inakuwaje Sekta Binafsi imekopa liingizwe katika Deni la Taifa? 33.6, ya Serikali 30.1 trilioni, lakini Deni la Taifa tunaambiwa ni trilioni 33.6. Deni hili la Taifa ina maana liko katika vichwa vyetu. Sasa nataka Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuja hapa anifahamisha inakuwaje trilioni 3.5 za Sekta Binafsi likawekwa katika Deni la Taifa? *(Makofi)*

Je, sisi ndiyo wadhamini ama Serikali ndiyo wadhamini wa deni hili la Sekta Binafsi? *(Makofi)*

Je, ikiwa hawakulipa hawa atalipa nani? *(Makofi)*

Hapa ni mambo ya kawaida, watafanya mchezo wao akishaambiwa kafilisika basi na kufilisika hapa ni rahisi tu. Hii itakuwa ni sahihi? *(Makofi)*

Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atueleze kwa nini Deni la Taifa linaingizwa na Deni walilokopa Sekta Binafsi?

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nasema ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante, wewe peke yako ndiyo umechangia bajeti, wengine huwa wanachangia vineno vineno. Umechangia bajeti, unastahili pongezi. *(Kicheko/Makofi)*

Nilisema Mheshimiwa Muhammad Chomboh, atafuatiwa na Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, Mheshimiwa Gregory Teu na Mheshimiwa Engineer Mfutakamba.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nguvu za kusimama na kupata nafasi hii ya kuchangia leo. Ninakushukuru wewe pia kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Waziri wa Fedha, kwa hotuba yake nzuri. Nampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), Mheshimiwa Mary Nagu, kwa Hotuba zao ambazo zilitupa mwelekeo

wa bajeti yetu ambayo imesomwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuangalia mustakabali wa kipindi kinachokuja cha mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja hii, lakini pia ninaomba kuisisitiza Serikali, kama ambavyo kwa mujibu wa taarifa aliyotuingia Mheshimiwa Waziri hapa, wamewekeana Mikataba na TRA katika kuhakikisha mapato yanafikia malengo yaliyokusudiwa ili kufanikisha bajeti hii iweze kutuvusha hapa ambapo tumejipanga. Hao ni wakusanyaji. Sasa nataka pia na Serikali na ninaiomba Serikali, iingie mikataba na watumiaji wa fedha hizo. Kwa sababu tatizo tunalolipata sasa hivi na linalolalamikiwa na Wabunge wote ni matumizi mabaya. Fedha zinapatikana, watumiaji kwa sababu tu hawana *commitment*, hawawajibiki na masuala ambayo wamekabidhiwa, wanatumia tofauti na matokeo yake malengo yaliyokusudiwa hayafanikiwi.

Kwa hivyo basi, kwa hatua iliyochukuliwa naipongeza sana Serikali hasa kwanza kwa kuweza kujitahidi safari hii kutotegemea sana wahisani, lakini kile ambacho wanategemea kupata kwa mapato na kuweza kuwekeana mikataba na wakusanyaji, kwa maana ya TRA, basi wahakikishe kila Wizara, kila Idara na kila Shirika, ambao wanakwenda kutumia fedha hizi kwa masilahi na kwa bajeti ilivyopangwa, wanawekeana mikataba na wahusika wa-deliver. Vinginevyo, wawajibike katika sehemu zao ili kuwe na nidhamu ya matumizi ya fedha hizi.

Tumechoka kila siku kulaumiana kwa kitu ambacho kinawezekana. Kama tunaweza kukusanya kwa nidhamu, kwa vyovyote vile lazima tuzitumie kwa nidhamu.

Nimefarijika pia kuona Miradi ya Maendeleo imepangiwa karibu trilioni 5.9, ambapo trilioni 4.3 ni fedha za ndani na trilioni 1.6 ni fedha za nje. Kwamba, angalau tumehakikisha kwa kiasi kukubwa sana fedha za maendeleo ni zile tunazozitegemea katika makusanyo yetu wenyewe badala ya kutegemea sana wahisani. Hiyo ni hatua mojawapo, kiasi ambacho ikiwa kweli Wafanyakazi wa Serikali wenye dhamana mbalimbali wakitekeleza wajibu wao ambao walikabidhiwa na waliwekeana mikataba na Serikali, tutafanikiwa. Tuna tatizo moja; Watanzania tunatakiwa tubadilishe mwono wetu kuwa, mtu akishapata na akishaajiriwa na Serikali basi hana ulazima wa kuwajibika, mwisho wa mwezi atapata mshahara, *whether* anafanya kazi atalipwa, hafanyi kazi atalipwa. Amefanya kazi saa kwa nane au saa kumi aliyopangiwa atalipwa na akifanya kazi kwa saa moja tu atalipwa. Tuachane na mtindo huo sasa.

Mimi ningeomba Serikali iwe na utaratibu wa wafanyakazi wote kila jioni kila mmoja ajitathmini, kuwe na sheria ya kujitathmini kutwa nzima muda ule ameufanyia kazi gani. Kionekane kile anachokifanya kinafanana na mshahara ambao analipwa kwa siku ile ama kwa mwezi ambao unafuatia. Hayo

yanatendeka katika sekta binafsi na ndiyo maana tunazungumza sekta binafsi zinakuwa na mafanikio kwa sababu wao wanamwajiri mtu kufanya kazi siyo kwenda kupata mshahara tu pale. Serikali inaajiri watu kwa ajili ya kuwalipa mshahara tu siyo kufanya kazi, tena wengine kwa ajili ya kwenda kuziiba na hizo hela zenyewe. Sasa hapo hapo hatutafika, Serikali inabidi ibadilishe Muundo huo tuliouzoa ndiyo tutafikia malengo na tutafika pale ambapo Wananchi watafaidika na masilahi yao.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kukisema tena kuhusiana na kodi ambayo Serikali imejitahidi, kodi ya wafanyakazi, sasa hivi inashuka na itakuwa vizuri ikifika mpaka *digit* moja, isiwe *percent* zaidi ya kumi. Lendeleee kila mwaka, hilo ni jambo zuri kwa sababu tunamwezesha mfanyakazi angalau kile anachokipata kipungue kodi kwa kila siku na kama kweli anawajibika kikamilifu. Hiyo sababu hali halisi tunaijua, Wananchi wetu wanapata shida na ni kweli hali ni ngumu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali pia ihimize na ijikite sana katika uzalishaji. Tunalalamika sasa hivi pesa yetu imeshuka bei, ni kweli pamoja na Dola kupanda bei huko kwao, lakini na sisi pia tumepunguza sana uzalishaji, tunanunua zaidi kuliko kusafirisha. Serikali iwe na mikakati madhubuti ya kuweza kuihami pesa yetu na njia pekee ni kutumia nguvu nyingi sana katika kuhakikisha uzalishaji unatendeka hasa kuhamasisha na kuiwekea mazingira mazuri Sekta Binafsi ambayo itazalisha kwa wingi kupitia viwanda. Kwenye kilimo hatujafanya chochote cha kilimo na tuna mgodi mmoja hatujautumia hata kidogo wa bahari.

Sekta ya Uvuvi, Serikali ya Tanzania au sisi Watanzania tumekuwa kama vile tumegubikwa. Tumezungukwa na bahari ambayo hatujaifanyia kazi yoyote na kuna fedha nyingi sana kule; sijui kwa nini Serikali kitu hiki hawajakiona?

Sisi wa Visiwani bahari ndiyo uchumi wetu kwa kila kitu. Pamoja na kwamba, kuna Mazao ya Karafuu na mengine, lakini Kisiwa chote kimezungukwa na bahari. Tunaijua bahari umuhimu wake na kuna nini kule ndani ya bahari. Sasa hivi kuna mwani, mwani ni zao mojawapo linalotoka baharini. Baharini kuna mambo mengine mengi sana ya kuweza kutuingizia kipato na Serikali ikaweza kupata mapato na ajira pia. Hebu tuache masihara na jambo hili, tuhakikishe mpango wa kuweza kuvuna mapato ndani ya Bahari Kuu unachukuliwa kwa umuhimu wake ili kuongeza kipato na Wananchi wetu na pesa yetu pia iweze kuhimili mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia, Serikali tunakokwenda tunakwenda katika kukabiliana na mambo ya uchaguzi. Uchaguzi una mambo mengi, ihakikishe usalama wa nchi yetu, kwa sababu kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, bajeti yote hii

itakwenda ikiwa usalama wa nchi yetu utakuwa mzuri na tunakwenda vyema. Wakati utakapofika wa kubadilishana uongozi kwa maana ya Uchaguzi Mkuu, twende kwa busara, lakini kuna ishara nyingine zinazojitokeza; kuna kiongozi ambaye aah, naona wenzangu wote wameondoka hapo, wale Wazanzibari wa upande wa pili, aah yupo mmoja. Kuna kiongozi mmoja juzi alitaka kuvunja Muungano, sana nia ya kuvunja Muungano. Kalizungumza hadharani, alikuwa anajificha ficha lakini juzi kalitoa hadharani kabisa kwamba, akipata yeye Serikali ya Zanzibar, kitu ambacho hakitatokea maishani mwake yeye, sijui huko baadaye, kuvunja Muungano pale Zanzibar.

Naamini Serikali itakuwa makini na kauli ile. Sisi wenyewe Wazanzibari tuko makini sana na kauli yake na tunalijua hilo siku nyingi, juzi tu kalitoa hadharani. Ninataka kuwahakikishia ndugu zangu kwamba, uchaguzi huu utakuwa salama na tutavuka salama kwenye Kura ya Maoni pia kwenye Katiba inayopendekezwa, itakapokuwa tayari sisi tumeshajiandaa. Bajeti hii tutaitumia katika kipindi cha 2015/2016 salama wala tusiwe na wasiwasi.

Serikali ihakikishe umakini huo unakuwepo, mambo madogo madogo haya yanayojitokeza yanakuwa yanadhibitiwa mapema, kwa sababu mtu akisema inawezekana ana nia kabisa ya kulifanya hilo. Sisi kwa maana ya Wazanzibari halisi tuko makini na hilo na tumejiandaa kukabiliana na lolote lile. Kuna aliyosema walimshauri akishapiga kura akalale nyumbani vijana wake watafanya kazi na sisi tuliishauri Serikali siku hiyo vijana wao wakikaa barabarani, Serikali ikae pembeni, vijana wengine watakaa barabarani. (Makofi)

Tunataka kuwahakikishia kwamba, itakuwa vizuri tu vijana kwa vijana, kila kitu kitakuwa *stable*. Usalama wa Zanzibar na wa Tanzania upo na tutapiga kura na tutapata ushindi, Chama cha Mapinduzi kitaendelea daima. Ninawashukuru sana Wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni, kwa kunionyesha tena faraja kwamba, wana nia nzuri sana ya kunirudisha tena hapa na Mungu akijaalia tutashirikiana tena na ninawaambia tutajaliwa na *Inshallah* Mungu atatujalia tutafanikisha na tutarudi tena kuja kuitetea nchi kwa masilahi ya Tanzania Zanzibar na Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. (Makofi)

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya mwisho katika Bunge hili kuweza kusimama mbele yako.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ndiyo mara yangu ya mwisho kuchangia katika Bunge hili, naomba nianze na shukrani za mtiririko. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyenipa nguvu na afya ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia nichukue nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, ukiwa kama mwanamke, kuliongoza Bunge hili kwa muda

wa miaka mitano sasa, kwa uvumilivu, kwa upendo, kwa hekima na maarifa, Mungu akubariki sana. Ningekuwa mimi nisingeweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii vilevile kuwashukuru sana wazazi wangu wapendwa, walionipa baraka za kuingia humu, na walionifundisha maadili ya kuheshimu kila binadamu mwenzangu bila kujali rika wala jinsia. Leo hii namaliza Bunge hili sina chuki na Mbunge yeyote mwenzangu, naongea na Vyama vyote bila kujali mipaka. Namshukuru sana Mungu. *(Makofi)*

Nawashukuru vilevile Viongozi wangu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, kwa kunipa nafasi ya kuingia katika Bunge hili pamoja na Wananchi, nimejifunza mengi na ninatoka sasa naelewa mengi; nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani nilizotoa, namshukuru tena mume wangu nilikuwa nimemsahau, mume wangu mpendwa Mr. John Mallac, kwa kunipa fursa ya kuwa mbali na yeye. Namshukuru sana kwa uvumilivu, lakini asijali, Mungu alimchagulia mimi ni mke mwema, ninayejitambua, ninaelewa maana ya mke wa mtu ni nini, kama nilivyokuja salama humu na ndivyo nitarudi salama; ahsante Mungu. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa nianze mchango wangu wa bajeti hii.

SPIKA: Umemuweka mwisho Mr. Mallac kusudi umseme vizuri. *(Kicheko)*

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mungu, kwa mume wangu Mr. John Mallac, kuniruhusu kujichanganya katika siasa na nikaweza kuchaguliwa kuingia humu. Asijali mimi kuwa mbali na yeye, naomba avumilie muda si mrefu nitarudi. Mungu alimchagulia mke mwema wala hakukosea. Ninajitambua, kama nilivyoingia humu salama na ndivyo nitarudi salama, kwa sababu najiheshimu, najua nini maana ya mke wa mtu. Ahsante sana Mungu. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa niende kwenye mchango wangu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii baada ya kuwa imeletwa mbele yetu, sasa muda siyo mrefu inapelekwa kwenda kukamilisha Miradi na mambo mengine kama ilivyopangwa. Napenda kuishauri Serikali ifuatilie na kuisimamia bajeti hii. Baada ya fedha kuanza kupelekwa katika Halmashauri, ifuatilie vizuri matumizi ya fedha yaende kwenye Mipango iliyopangwa.

Serikali isione haya kuwawajibisha Viongozi ambao ni wabadhirifu wa fedha za umma, kwa sababu hii ni faida ya Wananchi wote wa Tanzania. Serikali Isione haya kuwawajibisha Viongozi wazembe, wala rushwa na wenye

tamaa, kwa sababu hao ndiyo wanaoiangusha na kuichafua. Tumekuwa tukilaumu sana tunapona bajeti zinapangwa halafu Miradi haikamiliki. Mimi naongea kutokana na jioografia labda nianze na Mkoa wetu, bado tupo nyuma sana hasa katika suala zima la miundombinu ya barabara.

Naomba Serikali ituangalie kwa jicho la huruma Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma. Mikoa yetu ina fursa nyingi sana za kiuchumi hasa katika kilimo, madini na mazao ya biashara kama Tumbaku na Kahawa. Naomba sana barabara zifunguliwe kwa sababu ndiyo zinazofungua fursa za uchumi. Katavi tusipendwe tu inapoingia njaa magari yanakuja kule kubeba mahindi na mpunga ndiyo tunaonekana tuna thamani, hapana; naomba barabara zifunguliwe sasa tuwe na faida ya barabara kwa sababu tutatoa mazao mashambani kuleta kwenye masoko na vilevile mazao hayo yatatawanyika nchi nzima. Kwa hiyo, tunaomba sana barabara zikamilike katika mfumo mzima wa bajeti hii.

Barabara kwa kiwango cha lami kutoka Sumbawanga mpaka Mpanda, naomba ikasimamiwe vilivyo ili tuweze kupata matunda jamani. Vilevile Mpanda kwenda Kigoma kupitia Mishamo, ile barabara nayo ikamilike. Barabara kutoka Mpanda kwenda Tabora, yaani kiunganishi cha mikoa hii, tunaomba hizi barabara kuu mziangalie. Bila kusahau barabara za vijijini ambazo zinatoa mazao kwa urahisi kusogeza Mikoani sasa kwa ajili ya masoko.

Baada ya kusema hivyo, naomba Serikali muwakumbuke Wakandarasi walipwe pesa zao ili wafanye kazi kwa ufanisi na kwa kuzingatia viwango. Kazi zinalala, ile Miradi haikamiliki kwa sababu fedha zinachelewa kuingia katika Halmashauri kwa wakati na vilevile Wakandarasi wanachelewa kulipwa. Kwa hiyo, na wao kiwango kidogo walichonacho wanajenga barabara nyingine bila kuzingatia viwango, kwa kulipua. Ninaomba madeni ya Wakandarasi yakumbukwe, walipwe. Kwa upande wa barabara nimemaliza.

Naomba niende kwenye reli. Naomba Reli ya Kati jamani ikumbukwe. Reli ya Kati ikarabatiwe iunganishe mikoa vizuri na kuinua uchumi wa Mikoa yote ya Kanda nzima ya Kati. Wananchi wengi tunategemea sana reli, kwa sababu sasa hivi barabara hatuna inabidi malori yaje kule kupitia barabara na barabara bado zipo kwenye matengenezo, ndiyo kwanza zinazidi kuharibika. Kwa hiyo, tunaomba reli itengenezwe. *(Makofi)*

Vilevile tunaomba injini zenye nguvu. Nimewahi kuongea katika bajeti hii, nililalamika sana kuhusu injini mbovu tulizoletewa Mpanda. Wananchi ndiyo hasa wa kipato cha chini wanategemea kusafiri kwa treni, lakini treni ile ikiondoka haifiki kwa wakati, inalala njiani hata siku mbili, Wananchi wanasota njiani kwenye reli kwa sababu injini imeshindwa kabisa kupanda mlima! Kwa hiyo, naomba tukumbukwe tupate injini mpya.

Mheshimiwa Spika, naomba miundombinu ya elimu iboreshwe. Serikali ikumbuke sana, shule nyingi hasa vijijini ziko hovy. Wananchi wa vijijini naomba wakumbukwe kwani shule zao ziko hovy, madawati hayatoshi. Serikali imejitahidi kuongeza Walimu lakini bado hawatoshi. Pia, Wananchi wamejitahidi kujitolea kujenga maabara kwenye Shule za Sekondari za Kata zimekamilika, lakini umeme hakuna na maabara lazima vitumie umeme. Somo la TEHAMA, tunalihimiza lakini umeme hakuna vijijini. Naomba Serikali itimize maagizo yote iliyokuwa imeahidi, umeme utambae sasa vijijini. (Makofi)

Mawasiliano hakuna, kwa mfano, Kituo cha Afya cha Katuma hakina mawasiliano kabisa, inapotokea *emergence* mgonjwa anaumwa wanashindwa kuwasiliana na Hospitali Kuu. Naomba sehemu zilizokuwa zimebakia za mawasiliano kwa Mpanda kama Kata ya Katuma, Kijiji cha Kasekese, Sibwesa na sehemu zote, mawasiliano sasa yarekebishwe yafike kule ili Wananchi wafaidike.

Naomba sana Serikali inisikie kwa hayo maana ni kama narudia, kwa sababu nimeshayaongea kwenye Wizara zilizopita, ninachofanya sasa ni kuikumbusha Serikali kuihimiza.

Niende kwenye suala la afya na ustawi wa jamii. Maana ya ustawi wa jamii ni nini? Ni jamii kupata huduma zote stahiki kama vile elimu, maji na afya yenyewe. Huwezi kwenda shamba kulima kama wewe huna afya, huwezi kwenda darasani kama huna afya, huwezi kuingia Bungeni, Wabunge wengi viti vipo wazi wengine wana homa, huwezi kuingia humu kama unaumwa. Kwa hiyo, naomba afya ipewe kipaumbele kabisa. Vijijini huko Zahanati nyingi mlizohimiza kujenga wananchi wamejitolea lakini hazina madawa. Vituo ya Afya jamani havina madawa.

Naomba waganga waongezwe kwenye Vituo vya Afya ili Wananchi vijijini wanufaike. Hii nchi ni yetu wote, lakini Wananchi wa vijijini wanaishi katika mazingira magumu sana. Ukiangalia Katuma, narudia tena huko, Kituo cha Afya hakina mawasiliano, hakina maji, wanatumia maji ya visima. Kituo cha Afya cha Mwese hakuna maji na usafiri ni wa kusuasua. Naomba sana Serikali mote humo inusenuse ifanye marekebisho. Haya yote ni marudio kwa sababu nimeshayaongea.

Mheshimiwa Spika, kilio changu kikubwa hasa katika Wilaya ya Mpanda kilikuwa ni barabara na reli.

Mheshimiwa Spika, naona sina mengi ya kuongea, haya ni marudio. Bajeti isimamiwe, fedha zitumike jinsi ilivyopangwa. Serikali isimwonee haya mtendaji yeyote ambaye atachakachua hizi fedha, wala rushwa, wenye

tamaa, wazembe na wabadhirifu wa fedha Serikali, naomba iwe makini kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Gregory Teu, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Mikidadi na Eng. Mfutakamba baadaye!

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia bajeti ambayo ipo mbele yetu. Bajeti hii naomba ni-*declare interest* kabisa kwamba, mimi ni mdau kwenye Wizara hii ya Fedha, kwa sababu nililewa huko. Kwa hiyo, mengi ambayo nitayasema, naomba nitoe ushauri kwa Bajeti hii ya Serikali.

Kwanza kabisa, naomba nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa miaka mitano ambayo nimekuwepo hapa Bungeni. Nawashukuru wenzangu wote kwa ushirikiano ambao wamenipa. Nawashukuru Wananchi wangu wa Jimbo la Mpwapwa, kwa kuzidi kuniamini na kunipa ushirikiano wa hali ya juu katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ambayo ipo mbele yetu. Nawaomba wananchi wa Mpwapwa wakumbuke wapi wametoka, hivi sasa wako wapi na wanakwenda wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kumteua Mkuu wa Wilaya mpya ambaye ameingia hivi karibuni, ndugu yangu Mavunde, kuchukua nafasi ya Ukuu wa Wilaya. Naye ameahidi kwamba, kwanza, kufuatana na hali ya hewa ambayo siyo nzuri, atajaribu kupambana na suala la uhaba wa chakula kwa sababu mvua zilikuwa zimetutupa mkono.

Vilevile namshukuru sana Mkurugenzi wa Wilaya ya Mpwapwa, Mama Lusiga, kwa kazi nzuri ambayo anazidi kushirikiana nami ili kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Wilaya ya Mpwapwa, akishirikiana na Wananchi wote wa Mpwapwa, kwa kuunga mkono mambo yote ambayo yanafanyika.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Mawaziri wa Fedha wote wawili, Katibu Mkuu - Dkt. Likwelile na Makatibu Wakuu wote ambao wanasaidiana katika Idara hii, bila kuwasahau Wataalamu wa Wizara hii, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na kuweza kutoa bajeti ambayo ina kiwango cha hali ya juu. *(Makofi)*

Bajeti hii inatufundisha tuanze kujitegemea, jambo ambalo ni zuri sana. Vilevile napenda nichukue nafasi hii ambayo Wabunge wengi wakisimama naona kama walikuwa wamesahau kuikumbuka zaidi Ofisi ya Rais (Tume ya Mipango), ambayo imekuja na Mipango mizuri, ambayo ndiyo

itakayotekelezwa katika bajeti hii. Nawashukuru sana kwa Mipango mizuri kwa sababu inaonyesha kwamba, kama una Mipango mizuri tayari utakuwa umeshatekeleza bajeti 60%. Kwa hiyo, naipongeza Tume ya Mipango kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kutuandalia Mipango mizuri ya kutekeleza katika mwaka huu ambao tunaujadili hivi sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, zaidi nitajikita kushauri au utoa ushauri wa bure katika Wizara ya Fedha ili iweze kufanya vizuri. Kwanza kabisa, majirani zetu Wakenya ambao wana idadi ya watu milioni, 38 lakini bajeti yao ni trilioni 40.6. Sisi Tanzania tupo zaidi ya watu 46, lakini bajeti yetu ni trilioni 22.4. Unaweza kuona wenzetu wako mbele au sisi tupo nyuma tofauti hii inakuwaje au inakujaje?

Natoa ushauri wa bure hapo kwamba, kama wenzetu na asilimia ya bajeti yao, ukiangalia uwiano wa 38 na bajeti trilioni 40.6, sisi tukiwa chini watu wengi milioni 46 lakini bajeti ni 22.4. Ili kuikabili hali hii natoa ushauri wa bure kwamba, kwa upande wa bajeti ambayo inatekelezwa ambayo sasa hivi imeingia ya kuwashirikisha sekta binafsi, yaani PPP, ambayo ina Miradi ambayo inatekelezeka ndani ya nchi yetu.

Napendekeza kwamba, fedha chini ya taasisi hii ya sekta binafsi, yaani PPP, kama wanayo bajeti ya kutekeleza Miradi hii ya kiwango labda tuseme cha shilingi trilioni 20, napendekeza au ushauri wangu wa bure, haiwezekani kuzibuku fedha hizi zote za PPP chini ya Bajeti ya Serikali?

Kwa maana nyingine ni kwamba, kama Bajeti ya Serikali ni shilingi trilioni 22.4 na bajeti ya kutekeleza Miradi chini ya PPP labda ni shilingi trlioni 20, tujumlishe hii basi na sisi tutakuwa na bajeti ya trilioni 40. Tukielewa kwamba kuna mgawo wa PPP na mgawo wa upande wa Serikali ili tuonyeshe kwamba bajeti kitafsiri ni bajeti endelevu, bajeti ni lazima iwe *progressive*, inapanda kila mwaka. Haijalishi inapanda kwa kiasi gani lakini bajeti siku zote ni *progressive*. Tuone uwezekano wa kubuku pesa za maendeleo ambazo zinafanywa na Miradi chini ya utaratibu huu wa PPP nazo ziwe *booked* kwenye Bajeti ya Serikali ili tuweze kuongeza wigo wa bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nitoe ushauri ufuatao:-

Fedha za bajeti ya mwaka 2015/2016, zitolewe kwa miezi mitatu mitatu hususan bajeti ya maendeleo, badala ya kutolewa kwa mwezi mmoja mmoja. Hili nina makusudi kabisa kwamba, wakati bajeti inatolewa miezi mitatu na watu wanatumia au Wizara au Halmashauri inang'ang'ana kutumia fedha za miezi mitatu, Waziri wa Fedha atapata nafasi ya kutafuta tena fedha nyingine za miezi mitatu inayofuata.

Kama fedha haitoshi ya kutekeleza Miradi hii, basi akope kutoka Benki Kuu. Utaratibu wa kukopa Benki Kuu ni kwamba, unaweza ukatoa fedha miezi mitatu mapema kabisa mwanzoni mwa mwezi Julai, wakati fedha zile zinatumika miezi mitatu unapata nafasi ya kuwazia miezi mitatu ya mbele.

Gavana wa Benki anapotoa zile fedha ili zitumike kwa maana ya kuzikopa, ziende mapema katika Wizara zetu au Haramshauri. Yeye kwa sababu ndiyo anatunza Mfuko Mkuu wa Serikali, Waziri wa Fedha ana uwezo wa kutoa hati fungani kwa maana ya *bond* kwa Gavana wa Benki Kuu kwamba, tukopeshe pesa za kutekeleza Miradi ya miezi mitatu. Nawe unapopata pesa kuziingiza kwenye Mfuko Mkuu umeshika hati fungani, punguza pesa yako uliyoitoa mpaka utimize kufidia zile za miezi mitatu ambazo umekopesha. Hati fungani ile inakwisha baada ya yeye kupunguza kiasi kile mpaka mwisho. Akishapunguza fedha zile, hati fungani thamani yake imekwisha. Kwa utaratibu huu nafikiri itatusaidia kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Huo ni ushauri wa bure.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine ambao ningeusema ni kwamba, fedha zitolewe mapema kuanzia Julai ijayo. Waziri wa Fedha na Wataalamu wake akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara hii, wakae waangalie uwezekano wa kuandaa *Exchequer Issues* ambazo Mawaziri husika wote wanapotoka hapa wawe na *Exchequer Issues* za kuanza kutumia fedha hii tarehe 1 Julai, mapema kabisa. Zikitoka mapema kama ambavyo ninatoa ushauri, itakuwa inamsaidia sana Waziri wa Fedha; kwa sababu unapoanza mwaka wa fedha na wewe umeshatoa pesa za matumizi mapema hata kama kuna matumizi ambayo hayaeleweki yatajitokeza, wewe utakuwa salama kwa sababu umeshatoa pesa ile mapema kabisa. Najua kuna matatizo ya matumizi ambayo yanajitokeza wakati wa utekelezaji, lakini kama utatoa mapema miezi mitatu au mwezi mmoja kwa fedha ya kawaida (OC) na huku ukielewa hata matumizi ya aina yoyote yatakayokuja yatakuta wewe umeshatoa pesa na pesa ile inatumika, kwa hiyo utakuwa salama kabisa.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine ambao napenda niutoe ni kuhusu kushuka thamani kwa fedha yetu. Hili ni jambo kubwa, nchi nyingine za wenzetu thamani ya pesa kushuka ni *issue* kwa Waziri wa Fedha, kwa Gavana na hata Mkuu wa Nchi. Huko Ulaya kwenye fedha ya *Pound* ikishuka Waziri wa Fedha hata Mkuu wa Nchi anakuwa matatani. Huko Amerika, Dola ikishuka Mkuu wa Nchi, Waziri wa Fedha na Gavana wanakuwa mashakani. Sasa natoa ushauri wa bure kwamba, Waziri wa Fedha na Gavana msaidieni Rais, mchukue hatua madhubuti za haraka kukabili tatizo hili la kushuka kwa shilingi. (*Makofi*)

Sasa hivi Dola kwa moja ni karibu Shilingi 2,200/= hadi 2,300/= na inazidi kwenda mbele. Utakapokuja utueleze hatua za haraka ambazo unategemea kuzichukua kwa sababu ni suala kubwa sana katika nchi. Naomba ushauri huu

uuzingatie na utueleze hatua zipi ambazo mnatarajia kuzichukua ili kukabili tatizo hili la kushuka kwa thamani ya shilingi yetu sasa hivi inaenda kubaya. Hili ni jambo kubwa kama hatuna habari! Hili ndiyo tatizo ambalo litaleta hali mbaya ya maisha nchi hii, kushuka kwa thamani ya shilingi yetu. Kwa hiyo, tuichukulie hatua kali kabisa mwanzoni kabisa. Tukiacha itafika mpaka shilingi 3000/= kwa Dola moja, jambo la hatari kwako Waziri wa Fedha na Gavana, msaidieni Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ningekuwa na muda nilitaka nitoe shukrani, ulinichagua kwenda Bunge la Poland kuwakilisha Bunge la Tanzania kule, nilikuwa na wenzangu wasiopungua wanne tukaenda kule kuanzia tarehe 8 mpaka tarehe 13 Juni, 2015. Tumewakilisha vizuri, wale wenzetu kule walikuwa na mawazo tayari, walishakuja huku, wakaenda Mlima wa Kilimanjaro wakapanda kumbe walikuwa na madhumuni yao. Tumekuta wameandaa mkakati kwamba, wanataka kushirikiana na Afrika wanaita 'Go Africa.'

Nia yao ya kuja huku ilikuwa ni hiyo na wakatualika sisi tukaenda huko na wewe ukanichagua mimi nikaongoza ujumbe ule. Kule nimechaguliwa kuwa Mwenyekiti kwa upande wa Bunge la Tanzania na kule amechaguliwa Mwenyekiti wa Bunge la Poland, yaani Polish. Tunaandikiana mahusiano mazuri ya kushirikiana katika nyanja mbalimbali ikiwemo elimu, afya na maji. Wanataka watusaidie kuleta *wind-mills* na dawa kwenye hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ambalo nimeliona ni kwamba, lazima tufungue ubalozi na Poland. Ubalozi huu ulikuwepo mwaka 2008 lakini ukafungwa. Naomba niwasilishe ufunguzi wa Ubalozi wa Poland. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Utaniletea kwa maandishi hiyo taarifa yako. Tunaendelea na Mheshimiwa Fatma Mikidadi!

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika mjadala uliopo Mezani petu hapa leo. Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kuwatakia Waislamu wote kheri ya Mfungo wa Ramadhani.

Pili, napenda kuwashukuru Wananchi wa Mkoa wa Lindi, kwa kunipa ushirikiano mzuri katika kazi zote za Ubunge hadi kufikia leo. Nawashukuru akinamama na akina baba wote, kwa namna moja au nyingine akina baba wameweza kushiriki katika kufanikisha maendeleo ya kazi zangu za Ubunge.

Mheshimiwa Spika, vilevile nachukua nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote ambao tumeishi pamoja kama kijiji. Tulikuwa tunadhihakiana,

tunarumbana na kupeana pole na tumefanya kazi mbalimbali za Kibunge, lakini mwisho wa yote tunakuwa wamoja. Tulikuwa tunapeana majina hapa ukisema mtoto wa mkulima unajua ni nani, ukisema mama vicoba unajua ni nani, ukisema Tyson unajua ni nani; yaani huo ni ushirikiano ambao Wabunge wamekuwa wakifanya pamoja. Kuna Miss Bunge, kuna Mama Mjusi, kuna Yakhe, kuna Mama Chepechepe, kuna Mama Gender, kuna bwana vijisenti na majina mengi ya dhahaka, lakini wote tulikuwa tunafurahi, tunacheka na kufanya kazi zetu wote kwa pamoja kama kijiji. (Makofi)

Nichukue nafasi hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, tumefanya kazi vizuri kama walivyotangulia kusema wenzangu kwamba, kwa kweli ni mvumilivu, mstahimilivu na umefanya kazi kishujaa na mpaka tunamaliza Bunge mwezi huu. Wote nawashukuru, ahsanteni sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa niendeleo na ajenda iliyopo Mezani petu kuhusu bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika Mikoa ya Kusini hasa Mkoa wa Lindi, tumekuwa au tunalalamika miaka yote kwamba, Mikoa hii ni maskini. Tukawa tunaitwa kabisa kwamba, Mikoa ya Kusini ni maskini, Mikoa ya Kusini iko pembezoni, inaitwa sendelela kwa maana ya wakiwa, Mikoa ya Kusini ipoipo tu. Hii yote imesababishwa na baadhi ya Ajenda za Kimataifa kutotekelezwa vizuri. Kwa nini nimesema hivyo?

Nimesema hivyo kwa sababu kuna ajenda ziliwekwa na Jumuiya za Afrika inaitwa SADC. Ajenda ya SADC ilikuwa na maana ya kuendeleza Mikoa ya pembezoni au Mikoa ya Kusini. Mikoa hiyo ilikuwa Rukwa, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Pwani, Morogoro, Mtwara na Lindi. Mikoa hii iliwekwa katika Mkutano wa Mwaka 1997 kama Ajenda ya SADC ili kuendeleza Mikoa hii ya Kusini au Mikoa ya pembezoni. Mikoa hii ilikuwa na mpango wa kuendeleza biashara, kilimo, utalii, afya, uchimbaji madini, maji safi, umeme, mawasiliano, viwanda na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Ajenda hii ya SADC ya Mwaka 1997 haikuendelezwa ipasavyo na ndiyo maana Mikoa hii sasa inalalamika hatuna maji, umeme na kadhalika. Hii ni kwa sababu ajenda hii haikutekelezwa ipasavyo ili kuiwezesha mikoa hii kupata mafanikio ambayo sisi tulitaka yaendelezwe. Hadi leo tunaambiwa ni Mikoa maskini, Mikoa ya pembezoni au Mikoa sendelela kwa sababu hizi ajenda hazijatekelezwa ipasavyo

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali katika Bajeti hii ya leo itenge fedha ili Ajenda hii ya SADC iweze kutekelezwa katika Mikoa hii inayoitwa ya pembezoni au ya Kusini. Serikali iingalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, Ajenda ya SADC ilikuwa na maazimio 100. Maazimio haya 100 kwa Mikoa hii niliyoitaja isingelalamika hata kitu kimoja kwa sababu kila kitu kilikuwa kimepangwa ipasavyo. Ajenda ya kwanza ilikuwa ni kuendeleza barabara kutoka Manda mpaka Mchuchuma Project kwa ajili ya kusafirisha umeme kutoka Mchuchuma Village na kuunganisha umeme wa gridi ili uende katika machimbo ya Lake Victoria na Mikoa ya Mtwara Corridor; kwa maana ya Mikoa ya Rukwa, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Morogoro na Pwani. Hili lingetokelezwa tusingekuwa na malalamiko katika Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, ajenda nyingine ilikuwa kuendeleza Bandari za Mtwara, Manda, Mbamba Bay, Lindi, Kilwa na Bandari kadhaa muhimu zilizoko katika Mtwara Corridor. Naendelea kunukuu: "Kuendeleza Viwanja vya Ndege vya Mtwara, Songea na Njombe." Hivi vingekuwa vimeendelezwa, malalamiko mengi yasingekuwepo.

Barabara ya Mchuchuma hadi Mlimba, Daraja la Umoja wa Tanzania na Mozambique, naona hili limetokelezwa. Barabara ya Dar es Salaam – Kibiti – Lindi hadi Mtwara hii tunashukuru imetokelezwa. Reli ya Mbamba Bay hadi Mtwara hii inakuwaje? Tunataka tupate majibu. Reli ya Mtwara – Songea – Manda imekuwaje? Reli ya Manda – Mchuchuma – Mlimba imekuwaje?

Kupatikana kwa maji safi kwa Mikoa ya Mtwara na Lindi, tunataka Serikali itujibu hapa. Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa, Morogoro na Pwani maji safi vipi? Mawasiliano kwa Mikoa ya Mtwara Corridor.

Reli ya Tunduma – Sumbawanga – Kasanga na kuboresha barabara kwa njia ya changarawe imekwendaje?

Miradi ya Gesi ya Mnazi Bay, Mtwara, Gesi ya Kilwa na Songosongo mmeiendelezaje katika hili suala la Mtwara Corridor?

Mheshimiwa Spika, kuna Miradi zaidi ya 100, nikitaja hapa tutakesha. Ninachotaka kusema ni kwamba, kama Miradi hii iliyoidhinishwa Mtwara Corridor ingetokelezwa, tusingekuwa tunaitwa Mikoa ya pembezoni, Mikoa maskini na wala tusingeitwa Mikoa ya Sendelela.

Tunaomba Serikali iangalie Maazimio ya SADC ya mwaka 1997 yakatiwa saini tarehe 15 Januari 2004 yameendelezwa vipi. Tukikutana katika Vikao vya SADC au Afrika Mashariki yale Maazimio hayatekelezwi, hayaji hapa Mezani tukayaona?

Tunaomba Wizara husika iangalie upya suala la Mtwara Corridor ili liweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutotekelezwa Maazimio haya ambayo yanawekwa katika vikao mbalimbali vya SADC na kadhalika, ndiyo inapelekea sisi Mikoa ya Kusini kutoendelea hasa Mtwara na Lindi ndiyo tunapata tabu zaidi kuliko Mikoa mingine afadhali wanajivutavuta kuliko sisi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali iangalie mambo kadhaa ambayo Mtwara na Lindi tunapata shida tusaidiwe. Kwa mfano madini; Lindi tuna dhahabu, *gypsum*, *green tourmaline* na mambo mengi tu na unga wa rangirangi, lakini wachimbaji wadogowadogo hawajasaidiwa ipasavyo. Wanachimba madini haya kwa visu, majembe, nyundo na sululu. Serikali haijawaangalia ipasavyo, haijawapimia maeneo ipasavyo, hawajawezeshwa zana bora kama inavyosema Sera mpya ya Madini au Sheria mpya ya Madini ya mwaka 2010 kwamba, wachimbaji wadogowadogo wanapaswa wawezeshwe ili waweze kuchimba vizuri na kupata manufaa katika madini hayo. Tunaomba Serikali katika Bajeti hii iwaangalie hawa watu wa madini wa Mkoa wa Lindi hasa Wilaya ya Ruangwa kuna madini mengi, Liwale na Lindi Vijijini kuna madini mengi. Iende kule ikawape changamoto jinsi ya kuweza kuibua madini ambayo yapo pale.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, hii imepelekea sisi Mikoa ya pembezoni kutopata mawasiliano ya simu ya kutosha. Siku hizi simu za mkononi hutumiwa na wakulima, wavuvi, wafanyabiashara na watu wote. Je, Serikali inatusaidia nini sisi katika suala zima la minara? Kwa mfano, kule Lindi vijijini ndiyo kabisa, kuna vijiji kama Kiwawa, Rutamba, Kijiweni, Kilolambwani na Mvuleni, yaani hawa simu za mkononi wanazisikia tu hawana habari. Tunaomba Serikali iangalie kule, iangalie suala la mawasiliano Kusini, Liwale na Nachingwea. Watu angalie na sisi tunataka minara, kwa sababu watu wote sasa hivi wanatumia simu za mikononi. Kwa hiyo na sisi Kusini tusiendeleze haya majina ya kwamba hawa sendelela, wametengwa na nini; hapana, tuleteeni hiyo minara.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Umeme Vijijini (REA). Umeme wa REA upo sehemu nyingi tu nchini na sehemu zingine tayari wameshaanza kuutumia umeme wa vijijini, lakini Lindi bado. Vijiji vya Mkoa wa Lindi mpaka sasa watandika nyaya nguzo hazijasimamishwa. Sasa suala hili mpaka lini?

Tunaomba bajeti hii suala la umeme vijijini liendelezwe katika vijiji vya Mkoa wa Lindi, Nachingwea, Ruangwa, Liwale, Kilwa, Lindi Mjini na Lindi Vijijini tunataka umeme wa REA huko nako ufike.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, kuna suala la bandari. Bandari ya Lindi ilikuwa inafanya kazi nzuri sana. Ilikuwa inatoa ajira kwa Wananchi wa Lindi, lakini sasa haifanyi kazi yoyote imekaa tu pale. Wamekuja wakandarasi wakatengeneza

ndiyo kwanza wamezidisha umaskini, maji yamejaa na mchanga umejaa hata meli haiwezi kuweka nanga; kulikoni?

Tunataka Bandari ya Lindi ifufuke kwa sababu meli zilikuwa zinachukua bidhaa kutoka Lindi kupeleka Dar es Salaam na kuleta bidhaa Lindi na kupeleka maeneo mengine ya Songea, Tunduru na sehemu zote za Kusini kule. Vilevile watu walikuwa wanapata ajira kutokana na Bandari ya Lindi. Sasa hivi bandari imekufa, haipo na maji yanajaa yanakuja mpaka mjini, kwa sababu hakuna anayeangalia kwamba hapa ndiyo mwisho wa maji na hapa mwisho wa bandari. Maji yanapiga sasa yanakuja kujaza Mji wa Lindi, tutasikia tu baadaye Mji wa Lindi wote umefunikwa na maji kwa sababu hakuna anayeangalia bandari ile.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya Kusini ni bahari. Bahari inatoka Msumbiji kuja Lindi Tanzania kwenda Kenya. Inatoka Msumbiji inakuja Lindi, inapita Dar es Salaam inakwenda Kenya. Inapotoka Msumbiji inaleta samaki wengi wakubwa. Hivyo, ni vizuri ili tuweze kuwatumia samaki wale kuwe na kiwanda cha minofu ya samaki Lindi. Sasa Lindi tuna gesi lakini hatuna kiwanda hata kimoja hata cha samaki; samaki wanatoka Msumbiji wanakuja Lindi kuzaliana wanapita wanakwenda Mombasa. Samaki wengi sana wanakuja kuzalia pale Lindi, lakini hatuna hata kiwanda kimoja cha samaki. Tunaomba Serikali itusaidie.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Bibi Mijusi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Eng. Mfutakamba!

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nami naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Bajeti ya Serikali. Kwanza, nami niwatakie kila la kheri Waislamu wenzangu ambao wote tuko katika Mfungo wa Mwezi Mtukufu, Mwezi Msharraf wa Ramadhani na wale wengine wanaotusindikiza.

Mheshimiwa Spika, nianze moja kwa moja kuzungumzia suala la Reli ya Kati. Reli ya Kati ni mshipa au roho ya uchumi wetu katika Taifa letu, kwa sababu ukiunganisha na Bandari ya Dar es Salaam, tunahitaji udhibiti pamoja na uimara wa reli hii. Nitoe pongeze kwa Wizara ya Uchukuzi, kwa kuwa na ile *express train* na naomba treni ile isimame Goweko japo kwa dakika mbili pale Jimbo la Igalula, kwa sababu kuna uchumi mkubwa, kuna biashara nyingi; kuku, asali, *furniture*, mchele, karanga na mazao mengine. Itasaidia sana treni ile ikisimama japo dakika mbili, ili Wananchi pia wapande na kushuka. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la ujenzi wa Reli ya Kati. Kwa kweli kutoka Kaskazi, Tura, Malongwe, Goweko, Igalula, Karangasi, sasa hivi ile pauni themanini kwa *yard* imekamilika. Naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa umahiri wa kazi kubwa hii. Sasa hivi hata treni hazianguki kama ilivyokuwa zamani wakati reli ilikuwa nyembamba na mizigo inakwenda kwa wingi na kwa uharaka zaidi.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Chaya – Nyahua, kilomita 85, ninaipongeza tena Serikali ya Chama cha Mapinduzi, sasa hivi kutoka Kigoma mpaka Dar es Salaam zimebaki kilomita 85 tu ndiyo hazina lami. Mimi ninagari ndogo ya *facebook starlet* inakwenda mpaka Igalula sasa hivi, gari ndogo matatizo hakuna, usafiri umeimarika na ni wa lami; hongera sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ninaomba sasa Serikali ya Kuwait ikamilishe hiki kipande cha kilomita 85 kati ya Chaya na Nyahua na sisi tupate lami kwa sababu iko kwenye Jimbo la Igalula ili Wananchi sasa hivi watumie saa sita tu hadi saba kutoka Tabora mpaka Dar es Salaam kwa sababu ni lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la umeme. Jimbo la Igalula linaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, sasa hivi tuna umeme Loya, Tura na Lutende. Maeneo haya hata miaka ishirini ijayo umeme usingeweza kufika, kwa sababu zinahitajika nguzo kati ya 8,000 na 10,000 kupeleka kule, lakini Serikali sikivu, Serikali yenye kujali Wananchi wake, imeweza kutuletea umeme. Kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Igalula, nataka kuishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa umahiri huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, REA imekwishaweka utaratibu mzuri, sasa hivi Kata ya Kigwa, Kata ya Igoweko, Kata ya Igalula na Kata ya Nsololo, nyaya zimeshafika, vikombe vimeshafika, Wananchi wamekaa mkao wa kula wanasubiri tu umeme uwake. Tunaipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutuondolea kero ya giza.

Mheshimiwa Spika, nilibahatika kwenda Switzerland, nilikuwa na Mheshimiwa Mwijage. Tumefurahi sana kwa sababu Mataifa karibu 100 yaliyokuwa katika Mkutano Lusen karibu na Zurich, wamekubali Tanzania iwe *hub*, kwa sababu ya amani, utulivu na mshikamano. Kwa hiyo, sasa hivi kutakuwa na umeme wa Dunia (*Global Energy Internet*), utakwenda katika vijiji vyote vya Afrika na Tanzania ndiyo imechaguliwa kuwa *hub* na sisi tunaamini umeme huu utafanikisha kutuletea maendeleo ya haraka hata katika vijiji ambavyo havitakuwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, ninaingia katika suala la Bandari Kavu. Niseme masilahi yangu, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi Mkoa wa Tabora. Bandari Kavu ya Tabora ni muhimu sana, kwa sababu sasa tuna barabara ya lami inatoka Nzega inakuja Tabora, barabara ya lami inatoka Tabora

inakwenda Itigi, Barabara ya lami inatoka Tabora inakwenda Ipole mpaka Katavi, barabara ya lami inatoka Tabora inakwenda Urambo inakwenda Kaliua; hii ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi tuipongeze sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hizi barabara zinatoa fursa nzuri pamoja na reli iliyoimarika na uwanja wa ndege sasa wa lami Tabora, tuna kila sababu sasa ya kuwa na bandari ya nchi kavu kwa Mkoa wa Tabora. Serikali ya Mkoa wa Tabora imekwishatoa sehemu ambayo bandari kavu itajengwa, tuunganishe hizi bandari kavu na ya Kisarawe, Bandari Kavu ya Chalinze na Bandari Kavu ya Kigoma ili nchi mbalimbali zilizo jirani ambazo hazina bandari ziweze kuja kuchukua mizigo yao Tabora. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuanzishe kilimo cha mbogamboga na matunda kwa kutumia teknolojia nzuri ambayo tunapata kutoka SUA pale Morogoro ili tuweze kuzalisha mazao na ndege zije pale zichukue haya mazao kupeleka katika masoko mbalimbali ya Ulaya, Mashariki ya Kati na kwingineko, ambapo sasa lami ipo na ndege zitashuka bila tatizo lolote.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye mawasiliano. Ninaomba Vodacom, Airtel na Tigo watuletee mawasiliano. Vijiji vya Goweko, Nsololo, Mwitikila, Miziwaziwa, Kanala na Shekela, tuna tatizo la mawasiliano. Vilevile Isuli, kwa Kizengi, Tura, Nkongwa, Munyu, Lutona kuna Tigo lakini msukumo wake siyo mkubwa zaidi. Loya, Maguliati bado kuna tatizo, pia Lutende signal ni dhaifu. Male ambayo ni Kata mpya tunaomba pia mawasiliano yaimarike. Pia Miyenze pale Songambe ili tuweze kuwa na mawasiliano mazuri.

Mheshimiwa Spika, sisi ni wafugaji, tuna ng'ombe wengi kule tunataka tujue soko la Pugu sokoni ni shilingi ngapi kwa ng'ombe mmoja maksai. Tunapenda tujue bei kabla hatujamleta ng'ombe Dar es Saalam ili soko liwe zuri na mawasiliano ndiyo yanatusaidia kwa suala hili.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye ujenzi, tuna tatizo kubwa ninaiomba Wizara ya Ujenzi kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu, watusaidie lile Daraja la Nhwale. Nhwale inaunganisha Wilaya ya Igunga pamoja na Wilaya ya Uyui, kwa maana ya Jimbo la Igalula. Tukipata daraja hili litatusaidia sana kwa sababu Vijiji vya Muhama, Vijiji vya Itumba kwa Mheshimiwa Dkt. Kafumu kule na Mwamabondo wanategemea Loya Center pale kwenda hospitali.

Mto Nhwale huwa umejaa sana inakuwa hatari kwa akina mama wajawazito, halafu shule zote zipo Loya Center. Kwa hiyo, inakuwa shida kufika upande wa pili mto unapojaa. Daraja litatusaidia sana, ninajua TANROAD wamefanya upembuzi wa awali, lakini tunaomba zitengwe fedha ili tuweze kupata mawasiliano ya urahisi zaidi na maendeleo yapatikane kwa haraka. Loya wanashukuru pana umeme sasa hivi ni mbali sana.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye Bajeti ya Serikali. Ninaipongeza Serikali, PAYE imeshuka kutoka asilimia 12 kwenda 11, hiyo ni hatua nzuri. Pia mchele wa nje, kwa kweli mchele tunazalisha sisi pale lwembele, ni suala la package tu, mchele ni mwingi Bonde la lwembele. Kwa hiyo, kuweka asilimia 72.5 ya kodi ni sawa kabisa kwa mchele unaotoka nje. Tuimarisha wakulima wetu wa ndani wapate soko, wapate mchele. Najua maeneo mengine kama Mbeya kule wakati mwingine mchele nilikuwa ninapita ninaona uko kwenye maghala tu masoko yanakuwa shida kidogo.

Mheshimiwa Spika, pensheni ya wastaafu kutoka shilingi 50,000 kwenda 85,000 ni hatua nzuri lakini angalau iwe shilingi 100,000. Tujibane kidogo tuwasaidie hawa wananchi na Wazee wetu ambao wamesaidia sana katika maendeleo ya nchi yetu hii.

Mheshimiwa Spika, ningependa TATOA wazungumze na Wizara, kwa sababu nimeona wametoa malalamiko juu ya ongezeko la petroli. Wazungumze ili tuweze kuwa na ushindani mzuri wa kusafirisha, ukilinganisha na gharama ambazo wenzetu Afrika ya Kusini, Namibia, Mozambique pamoja na Zambia, ushindani wa usafirishaji uwe na mwelekeo ambao unaweza kuwa wa kusaidia hawa wamiliki wa usafirishaji wa TATOA.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waziri wa Fedha na Manaibu wake, lakini pia Wananchi wa Igalula, kwa kuendelea kuniadini, wanirudishe tu mimi ni jembe na wao wanajua. Wale wengine wapige porojo tu lakini hakuna tatizo. *Inshallah*, nitarejea Bungeni tena ifikapo Novemba.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wale wote waliotakiwa kuchangia leo wamemalizika, kwa hiyo, Siku ya Jumatatu tutaanza na Mawaziri mbalimbali kujibu hoja ambazo Wabunge walikuwa wanazitoa katika kipindi hiki. Kama nilivyosema, Vyama vyote mhakikishe Wabunge wenu wote wanakuwepo tarehe 23 humu ndani, maana tutapiga kura za majina.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa sina matangazo mengine, ninaahirisha Kikao cha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

(Saa 12.49 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 22 Juni, 2015, Saa Tatu Asubuhi)